Ijumaa Julai 19, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581742

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



**MBAPPE: SIHOFII KUCHEZA NA VINICIUS JR REAL MADRID** UKURASA 21

UKURASA 4

**Saa** tatu, dakika 25 treni SGR Dar - Dodoma



UKURASA 4

**NIDA** yatoa ufafanuzi matumizi ya namba za taifa

UKURASA 7

**Kutokula** chakula kwa muda mrefu hatari kwa afya

# Migogoro ardhi inavyozibomoa familia nyingi

• **Kesi** 600 zapokewa kwa wiki Kituo Jumuishi Temeke ... *Endelea ukurasa 2*



Mary Makondo



# Mtaalamu anavyoonja vikombe 1,000 chai na kubaini ladha tofauti

UK. 12

UKURASA WA 4

## KIJANA ANUSURIKA KUUAWA KWA MADAI YA WIZI WA NGUO

KIJANA Husseni Juma, anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka 20, amenusurika kuuawa ...

UKURASA 3

## Samia: Tuzike tofauti zetu, tuanze upya



**MICHEZO** **YANGA YAENDA SAUZI NA BALEKE** UK.24

**MAONI,** UK.6

# CRDB, Water.Org kuboresha miradi ya maji na usafi

Na Mwandishi Wetu

BENKI CRDB imetia saini mkataba wa makubaliano na shirika la Water. Org Afrika unaolenga kuboresha upatikanaji maji safi na mazingira safi katika maeneo mbalimbali nchini.

Akizungumza katika hafla ya kutia saini makubaliano hayo jana jijini Dar es Salaam, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB na Ofisa Mkuu wa Uendeshaji wa benki hiyo, Bruce Mwile alisema makubaliano hayo ni sehemu ya utekelezaji azma ya Benki ya CRDB ambayo inaelekeza katika kutoa suluhisho bunifu kwa jamii ili kukuza ustawi wa wadau wake.

"Tunajivunia kuona tunaendelea kuishi azma yetu ya kuchochea ustawi wa jamii kupitia ubia wa kimkakati na wenzetu wa Water.Org. Nizishukuru timu zetu za kitaalamu ambazo zimefanya kazi kubwa hadi kufikia hatua hii ambayo inatoa fursa kwa jamii kunufaika na uwezeshaji katika sekta ya maji na usafi," alisema Mkurugenzi huyo.

Mwile alisema ushirikiano huo utawezesha miradi ya sekta ya maji pamoja na usafi wa mazingira kwa kutumia fedha zitakazotengwa katika maeneo mbalimbali. Miongoni mwa maeneo hayo ni utafiti na ufadhili wa miradi ya maji na usafi wa mazingira, mikopo ya miundombinu ya maji na usafi.

Benki hiyo intarajia pia kutoa mikopo midogo kwa watu binafsi, wajasiriamali, biashara na taasisi kwa ajili ya kufunga miundombinu ya maji ya nyumbani, vifaa vya matumizi ya maji kwa ufanisi na ujenzi wa vyoo na matangi ya maji safi na maji taka.

Alisema mikopo hiyo pia itaelekezwa katika sekta ya kilimo hususani kwa wakulima wanaotumia mifumo ya umwagiliaji yenye matumizi ya maji kwa ufanisi, pia kuwezesha uanzishwaji huduma za bima zitakazotoa ulinzi dhidi ya majanga yanayoathiri miundombinu ya maji.

Mkurugenzi Mkuu Water.Org, Francis Musinguzi alisema ushirikiano huo unalenga kuboresha maisha ya jamii inayowazunguka pamoja na kuwezesha ufadhili wa utafiti wa hatifungani za maji na usafi wa mazingira, pamoja na kuanzishwa kwa miradi endelevu ya maji na usafi.

"Ushirikiano huu pia utawezesha ufadhili wa utafiti wa ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi katika kufadhili miradi mikubwa ya usambazaji maji na usafi, pamoja na ufadhili wa bunifu za usimamizi wa maji kwa teknolojia," alisema Musingizi.

Katika eneo la elimu na uhamasishaji, Benki ya CRDB na Water.Org watashirikiana kufadhili kampeni za elimu na uhamasishaji kuhusu umuhimu wa usafi ili kuzuia magonjwa kupitia taasisi ya CRDB Bank Foundation ambayo imejikita zaidi katika kutoa elimu kwa jamii na kutoa mitaji wezeshi kwa wajasiriamali wanawake na vijana.

Makaubaliano ambayo Benki ya CRDB imeingia na Water.Org ni mwendelezo dhamira ya benki hiyo kuchangia ufikiaji Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs), hususan Lengo Na. 6, 'Maji Safi na Usafi wa Mazingira'.

# Migogoro ardhi inavyo bomoa familia nyingi

Na Elizabeth Zaya

MIGOGORO ya ardhi ni tatizo kubwa kitaifa: Familia nyingi zimeparanganyika kutokana na ndugu kugombea ardhi.

Sikia ushuhuda huu wa Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Msaada wa Kisheria Wizara ya Katiba na Sheria, Ester Msambazi:

"Tangu tuanze kampeni hii ya kutoa msaada wa kisheria, tumekutana na mambo mengi, wakati mwingine tunalazimika kutembea umbali mrefu kuwafikia wananchi kutatua migogoro kuhakikisha hatuachi iendelee tena.

"Ninaweza kusema kwamba bado tuna kazi kubwa ya kufanya. Kuna migogoro kwenye familia kati ya ndugu na ndugu, jirani kwa jirani na hata taasisi za umma na wananchi hususani kwenye masuala ya ardhi, mirathi, ndoa na ukatili."

Ester ni miongoni mwa maofisa walio katika timu ya wanasheria na wabobezi wa sheria ambao wamekuwa wakizunguka kutoa msaada wa kisheria katika mikoa mbalimbali nchini kupitia kampeni ya kitaifa ya msaada wa kisheria iliyozinduliwa mwaka jana. Timu hiyo tayari imeshatoa huduma kwa wananchi 490,000 katika mikoa saba.

Katika mazungumzo na Nipashe, Ester anasimulia migogoro waliyokutana nayo, akiwa na angalizo kuwa jitihada zinapaswa kuongezwa kuwasaidia wananchi katika eneo hilo kwa kuwa migogoro katika jamii ni mingi.

Anasema wapo baadhi ya ndugu ambao wamefarakana na wengine hata kutishiana kuuwana kutokana na migogoro inayotokea katika familia zao.

"Si tu kwa familia, migogoro mingine inatokea kati ya majirani au taasisi za umma na wananchi ambayo inafikia wakati kusababisha mfarakano na kuhatarisha amani kati yao," anasema.

Ester Akitolea mfano mgogoro wa ndugu ambao umedumu kwa zaidi ya miaka 10, wakigombania kipande cha ardhi walichogawiwa na baba yao mzazi na wamekuwa hawasalimiani na wakati mwingine kutishiana kuuana mpaka walipopatanishwa na timu hiyo ya wanasheria.

"Huu mgogoro tulikutana nao Kata ya Bonga, Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, Ni wa mirathi ambao ulikuwa umechukua zaidi ya miaka 10, ukihusisha ndugu watatu wa kiume wa baba na mama mmoja. Baba yao alishafariki dunia, wakabaki na mama yao mzazi ambaye wanaishi naye.

"Tulipokuwa tumekwenda kwenye mkutano wa hadhara katika kata hiyo kutoa elimu maana huwa tunafanya mkutano na tukimaliza tunaita mtu mmoja mmoja tunamsikiliza. Tukawa tumepokea mgogoro wa mtu anayelalamika kwamba amezuiliwa kuishi nyumbani kwake na ndugu zake na alikuwa na alama za mapanga kwenye mwili wake.

"Alisema amekuwa akitumiwa watu na anaodai kuwa ni ndugu zake kwenda kumjeruhi na ana kesi mahakamani ambazo amesingiziwa na hao ndugu zake," Ester anasema na kueleza kuwa mgogoro huo ulivuka mipaka na kuhusisha watoto wa pande hizo, nao wakawa na uhasama, hata kutosaidiana kwa lolote.

"Akatueleza zaidi kwamba amezuiwa hata kwenda kwa mama yake na wamejenga uzio ili asivuke kwenda upande wa pili kwa mama yake licha ya kwamba ni jirani na ana shamba huko," Ester alieleza zaidi kuhusu mgogoro huo.

Anasema kuwa baada ya kumsikiliza ilibidi wamwite Ofisa Mtendaji wa Kata ambaye alithibitisha kuwa na taarifa za mgogoro huo wa muda mrefu na akakiri ameshindwa kuutatua, hivyo timu hiyo ikaingilia na kuutatua.

"Tulikwenda pia mahakamani tukamfuata hakimu na kumwomba asilitolee suala hilo uamuzi ili tujaribu kuusuluhisha kwanza, tulipokutanisha pande hizo, msuguano ulikuwa ni mkubwa, tulitumia njia za utatuzi wa migogoro ambazo wakati mwingine unatoa mmoja unabaki na mwingine kwa sababu kila mtu alikuwa na jazba," anasimulia.

Anasema walipofika eneo la tukio, walikubaliana kupima eneo hilo ili kufahamu nani mwenye eneo kubwa na nani mwenye eneo dogo.

Anasema kwamba baada ya kupima waligundua kwamba eneo la mlalamikaji lilikuwa kubwa kuliko maeneo ya wale wengine wote na wakatatua mgogoro huo kwa njia ya usuluhishi.

Nipashe ilizungumza na mmoja wa ndugu hao waliokuwa wakigombana, Safari Bura ambaye alisema tangu wasuluhishwe na wanasheria hao, sasa wanaishi kwa amani.

"Hali ilikuwa mbaya sana, tumeishi kwa muda mrefu bila hata kusalimiana, tulikuwa tunawindana, kuna mmoja wetu alishindwa hata kushiriki mazishi ya mzee wetu, akihofia usalama wake, lakini tunashukuru sana, kwa sasa tuko huru kabisa, amani imetawala," alisema Bura.

Alishauri, "Tunaomba kazi inayofanywa na timu hiyo iendelee, kama sisi tulikuwa na tatizo hilo, ninaamini wapo wengine wengi huko ambao watahitaji msaada kama tuliopata sisi."

Kwa mujibu wa Ester, migogoro iliyojitokeza kwa wingi katika mikoa yote waliyopita ni pamoja na ya ardhi, mirathi, ndoa na ukatili.

Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Mary Makondo, alisema taarifa alizopewa na Kituo Jumuishi cha Mahakama cha Temeke, zinaonesha wanapokea zaidi ya kesi ya


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD, TRUST RECOVERIES LTD, BEST GROUP (T) LTD, JAMOK INVESTMENT LTD,MCHINGA AUCTION MART,GADAU AUCTION MART,AMI AUCTION MART, IGALULA AUCTION MART,BAHARI AUCTION MART, ADILI AUCTION MART,KOTI BROTHERS CO. LTD,PROPERTY MASTER LTD,MULTILINK AGENCY LTD,TWINS AUCTIONS MART, BID CITY AUCTION,JALAS AUCTION MART,HOLLYNESS COMPANY LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| KARIAKOO | GOGADI DISPENSARY LIMITED | NYUMBA | MARTHA BAGOME GOGADI | PUGU KINYAMWEZI | 05/08/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | PADONI KIBAYU SIMON | NYUMBA | PADONI KIBAYU SIMON | PUGU KINYAMWEZI | 05/08/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| DODOMA | KOLE JOSEPH SAINI | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | KOLE JOSEPH SAINI | BOMBAMBILI ILALA DAR ES SALAAM | 23/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| DODOMA | NICHOLAUS DEOGRATIUS MUHAGAMA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | ANNA MANYANGU MADUHU | NKUHUNGU | 23/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | DOREEN JAMES TEMBA | NYUMBA | DOREEN JAMES TEMBA | KIPUNGUNI-ILALA | 24/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | ALLY SHAWEJI OMARY | NYUMBA | ALLY SHAWEJI OMARY | LUGURUNI-KIBAMBA | 02/08/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TANDALE | MAIMUNA ISAYA KIRINDO | NYUMBA | MAIMUNA ISAYA KIRINDO | KIMARA | 05/08/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.

2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.

3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0714939933/0759648448/0715868000/0765999000/0714208208**

4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

HABARI KITAIFA

# Samia: Tuzike tofauti zetu, tusonge mbele

**Na Joyce Lameck**

RAIS Samia Suluhu Hassan amevitaka vyama vyote vya siasa kuingia katika falsafa ya kuweka kando tofauti zao na makosa yaliyowahi kutokea nyuma ili kuimarisha mshikamano katika kujenga taifa.

Awali, Mbunge wa Viti Maalum, Stella Fiayo, alimweleza Rais Samia kwamba baada ya uchaguzi wa mwaka 2020, vijana wengi walitoka Tanzania na kwenda kuishi nchi jirani ya Zambia lakini sasa wamerejea kuendelea na ujenzi wa taifa.

Alizungumza jana mkoani Songwe ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake, Rais Samia pia alisisitiza Watanzania kuwa na umoja, ushirikiano katika kuleta maendeleo kwa taifa.

Mkuu huyo wa nchi alisisitiza Watanzania kutokwepa ulipaji wa kodi ili kuwezesha nchi kupata maendeleo akisema ulipaji mzuri wa kodi ndio unaofanya pato la taifa kuwa kubwa na kufanya mambo kwa ukubwa zaidi.

“Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni moja tu, hivyo Watanzania tuwe wamoja ili kutimiza hilo. Tulikuja na falsafa ya vyama vyote vya siasa tuwe na maridhiano, tusameheane, twende kwa umoja katika mabadiliko na taifa kulijenga kwa uzuri.

“Ndugu zangu mazuri yote haya yaliyotajwa hapa yanafanywa na kodi.

Ninakubali kuwa wakati mwingine tunaowaamini kukusanya kodi wanakosea, hilo tumeliona na tunalifanyia kazi, lakini ninawaomba kila mmoja alipe kile anachotakiwa kulipa katika kodi, ili twende na mtiririko wa kujenga taifa letu,” alisema.

Awali, Mbunge Fiyao alisema Rais Samia amefanya thamani ya mwanamke kujulikana duniani katika uongozi na kufanya kazi.

Alimpongeza Rais Samia kwa jitihada kufanya watanzania kuungana na wakazi wa Tunduma kuwa kitu kimoja, kuishi kama ndugu ukilinganisha na kipindi cha nyuma.

Mbunge huyo alisema kipindi cha nyuma hakukuwa na ushirikiano katika jambo lolote, lakini tangu Rais Samia aingie madarakani amefanya wawe kama ndugu.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, aliahidi kutatua changamoto ya maji katika Mkoa wa Songwe kwa kutekeleza ahadi ya kiapo alichoapa kwa Rais.

Waziri Aweso aliahidi kuwa watatumia Mto Momba ili kusambaza maji safi na salama katika maeneo ya Tunduma na mengine.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema Septemba Mosi, mwaka huu, serikali itatangaza bei mpya ya mbegu za mahindi itakayouzwa kwa ruzuku, huku akisema gunia la mahindi litauzwa kwa Sh. 70,000 badala ya Sh. 42,000 ya awali.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Selemani Jafo, aliahidi kuongeza idadi ya viwanda vya uzalishaji katika Mkoa wa Songwe na kuweka mifumo mizuri ya wafanyabiashara kuweza kusafirisha bidhaa bila ya kuwapo kwa changamoto kwa nchi jirani.

Naye Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, aliahidi kutekeleza ujenzi wa barabara ya Tunduma-Mbeya kwa haraka ili kurahisisha safari za kibiashara kufanyika bila kikwazo chochote.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, akijibu moja ya bango la wananchi waliloomba kujengewa kiwanja cha kisasa cha mpira wa miguu, alisema serikali itatoa takriban Sh. milioni 300 kwa ajili ya kutekeleza hilo.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Daniel Chongolo, alisema pamoja na uboreshaji elimu kwa shule za msingi na sekondari, kumekuwa na changamoto ya ongezeko kubwa la mimba za utotoni mkoani humo.

Hata hivyo, Chongolo alimhakikishia Rais Samia kuwa ndani ya mwaka moja atarajie kuona mabadiliko kuhusu suala hilo, kwani tayari ameshaanza kulifanyia kazi katika maeneo mbalimbali.

# Vitalu vipya mafuta, gesi asilia kutangazwa

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), inatarajia kutangaza vitalu vipya vya uchimbaji mafuta na gesi asilia ambavyo vimebainika baada ya kufanya utafiti wa awali katika maeneo mbalimbali nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa PURA, Charles Sangweni, alisema utafiti huo unaonyesha kuwa asilimia 50 ya eneo lote la nchi lina miamba tabaka yenye mafuta na kwamba miongoni mwa maeneo ni ukanda wa pwani, kati na Nyanda za Juu Kusini maeneo ya Mbeya.

“Kwa hiyo matarajio hayo ya kutangaza vitalu vipya ni baada ya utafiti wa awali ambao tumeufanya katika maeneo mbalimbali ya nchi yanayoonyesha viashiria vya uwapo wa mafuta na gesi asilia.

“Tunategemea mwaka huu mwishoni au mwanzoni mwa mwaka ujao, tutaweka bayana maeneo mbalimbali ambayo tutavutia wawekezaji kwa ajili ya kushirikiana nasi bila kusahau Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwenye kutafuta na ikiwezekana tutakachokipata kukiendeleza na kukizalisha,” alisema.

“Kwa sasa mambo yanabadilika kwenye matumizi ya nishati dunia yote inaongelea nishati safi na sasa inaondoka kwenye matumizi ya nishati ya petroli kwenda kutumia nishati inayozuia uchafuzi wa mazingira.

Tanzania tumeweka malengo ya kutumia nishati safi ya kupikia kwa kufikia hadi asilimia 80 ifikapo mwaka 2034,” alisema Sangweni.

Utafiti huo wa awali ambao wamefanya katika maeneo mbalimbali ya nchi, alisema unaonyesha maeneo yenye viashiria vya kuwapo mafuta takribani kilomita za mraba 534,000 ambazo ni zaidi ya asilimia 50 ya eneo lote la Tanzania.

“Liko eneo kubwa lenye miamba tabaka yenye viashiria vya uwapo wa mafuta na gesi asilia ambalo bado hatujafanyia utafiti tunaloamini kwamba huenda likawa na viashiria vya rasilimali hiyo,” alisema.

Sangweni alisema katika kutangaza fursa hizo, wataanza na ukanda wa pwani kisha kuendelea maeneo mengine yakiwamo Singida na Kyela mkoani Mbeya.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza “subscribe”
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona “E-Paper” utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Kijana anusurika kuuawa kwa madai ya wizi wa nguo

**Na Tuntule Swebe**

KIJANA Husseni Juma, anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka 20, amenusurika kuuawa baada ya kushambuliwa kwa kipigo kwa tuhuma za wizi wa nguo.

Juma alikumbwa na mkasa huo juzi asubuhi maeneo ya Tegeta, Dar es Salaam, baada ya kukutana na mtu aliyedai nguo alizokuwa amevaa ni zake.

Mashuhuda waliiambia Nipashe kwamba tukio hilo lilitokea majira ya saa 3:00 asubuhi na kijana huyo alijitetea kwamba ni nguo zake na alinunua wakati mdai akisema ni zake kwa kuwa ziliibwa mahali anapoishi.

Katika utetezi wake, Juma alijitetea kwamba alinunua nguo hizo kwa mwenzake aliyemtaja kwa jina la Kuchi.

Shuhuda ambaye hakutaja jina lake litajwe gazetini, alisema kijana huyo alikimbizwa kutokea Tegeta Machinjioni hadi nguzo za Zanzibar na wananchi baada ya kudaiwa amevaa nguo za wizi.

"Alipigwa na baadaye walitaka kumchoma moto lakini hawakufanikiwa kwani alijitetea kwa kukimbia lakini jitihada zake hazikufanikiwa kutokana na majeraha aliyokuwa nayo," alisema.

Kwa mujibu wa shuhuda , kijana huyo alijeruhiwa maeneo mbalimbali ya mwili ikiwamo kichwani.

Kaimu Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Tegeta kwa Ndevu, Amos Chuma, alisema kijana huyo ni mkazi wa Salasala japokuwa awali alikuwa akiishi Tegeta huku akibainisha kuwa alikuwa anafanya kazi ya kuendesha bodaboda.

Kijana mwingine, alimtetea Juma akidai kwamba si mwizi na kwamba anapata kipato kutokana na kazi yake ya bodaboda.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na mgeni wake, Balozi wa Switzerland nchini, Dider Chassot (wa pili kulia), Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Saa tatu, dakika 25 SGR Dar-Dodoma

**Na Restuta James**

TRENI ya mwendokasi katika reli ya kiwango cha kimataifa (SGR) kuanzia Dar es Salaam hadi Dodoma, zinatarajiwa kuanza Alhamisi ijayo huku zikitegemea kutumia saa tatu na dakika 25 kwa safari nzima.

Aidha, kuanza kwa treni hiyo kutaathiri treni ya kawaida ya SGR inayofanya safari zake kuanzia Dar es Salaam hadi Morogoro.

Taarifa ya Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano katika Shirika la Reli Tanzania (TRC), Jamila Mbarouk, kwa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam jana, ilisema safari ya treni hiyo itaanza Julai 25, mwaka huu, na kwamba itaondoka Dar es Salaam saa 12:00 asubuhi na kufika Dodoma saa 3:25.

Taarifa hiyo ilisema treni ya kawaida ya SGR ya Dar es Salaam - Morogoro iliyokuwa inaondoka saa 12:00 asubuhi sasa itaondoka saa 3:30 asubuhi.

"Treni ya haraka (express train) itatoka Dar es Salaam saa 12:00 asubuhi na itatoka Dodoma Saa 5:30 asubuhi. Treni ya kawaida kutoka Dar es Salaam Kwenda Morogoro itatoka Dar es Salaam saa 3:30 asubuhi na saa 10:00 jioni, itatoka Morogoro saa 3:50 asubuhi na saa 10:20 jioni," alisema.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, safari za treni zote zitakuwa kila siku bila kujali mwisho wa wiki au siku za kazi.

Katika taarifa hiyo, Mbarouk alisema tiketi za treni zote zinapatikana kwa njia mtandao (online) na katika stesheni za SGR.

Treni ya haraka ya Dar es Salaam hadi Dodoma inaanza ikiwa ni mwezi mmoja na siku 11 tangu kuanza kwa safari za treni ya SGR kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro, zilizoanza Juni 14, 2024.

Treni hiyo ya haraka itasimama Morogoro pekee na kisha Dodoma, wakati ile ya kawaida itasimama katika vituo vidogo kikiwamo cha Pugu.

Nauli za treni ya kawaida Dar es Salaam hadi Dodoma (km 444) zitakuwa Sh. 31,000 wakati ile ya haraka ni kati ya 70,000 na 120,000 kulingana na daraja abiria analochagua kati ya biashara (business) na la juu (royal).






# NIDA yatoa ufafanuzi matumizi NIN

**Na Restuta James**

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), imetoa ufafanuzi kuhusu matumizi ya namba ya utambulisho wa utaifa (NIN) na kitambulisho cha taifa huku ikieleza kuwa yanakwenda sambamba.

Akizungumza jana katika ofisi za Nipashe, Dar es Salaam, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa NIDA, Geoffrey Tengeneza, alisema pamoja na kwamba wananchi wengi bado hawajachukua vitambulisho vyao, wataendelea kupata huduma mbalimbali kupitia namba zao za kitambulisho kinachotolewa na mamlaka hiyo.

"Nimeona nitoe ufafanuzi kuhusiana matumizi ya namba za utambulisho wa taifa (NIN). NIDA hatujasitisha matumizi hayo na hatuna mpango wa kuyasitisha kwa sababu namba hizi ni muhimu kwa wananchi kuendelea kupata huduma," alisema.

Tengeneza alisema NIDA inafahamu kuna wananchi wenye vitambulisho na wengine hawana kutokana na changamoto mbalimbali, hivyo NIN inawawezesha kupata huduma.

"Kwa hiyo hatujasitisha, cha msingi tunatoa tu msisitizo kwamba kwa kuwa tuna vitambulisho vingi ambavyo tumevizalisha na tumevipeleka hadi ofisi za serikali za mitaa, vitongoji na shehia.

"Wananchi wajitokeze kuchukua vitambulisho vyao hata kama mtu ana namba tayari badala ya kuridhika kwa sababu ana namba na anapata huduma," alisema.

Alisema mwananchi kupata kitambulisho hicho ni haki yake na kwamba kitaendelea kutumika kupata huduma muhimu kama inavyotumika NIN hivi sasa.

NIDA imetoa ufafanuzi huo wakati ambao kuna mrundikano mkubwa wa vitambulisho vinavyotolewa na mamlaka hiyo ambavyo vipo katika ofisi za serikali za mitaa, kata, vitongoji, vijiji, wilaya na mikoa.

Taarifa zinaonyesha kwamba mkoa wa Dar es Salaam una idadi kubwa ya vitambulisho kwa kuwa watu wengi hawajaenda kuvichukua.

HABARI KITAIFA

# Mabomu ya machozi yatumika kutawanya wachimbaji wadogo

**Na Ambrose Wantaigwa,**
BUNDA

JESHI la Polisi wilayani Bunda, jana lilitumia mabomu ya machozi kuwatawanya wachimbaji wadogo waliofurika katika ofisi ya kijiji cha Kanyambiga kwa madai ya kunyang'anywa maeneo yao na kupewa mwekezaji.

Kutokana na tukio hilo, Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Vincent Naano, aliwataka wachimbaji hao kufuata sheria wakati wa kudai haki dhidi ya mwekezaji wa mgodi katika kijiji hicho.

Aidha, Naano alikemea baadhi ya wanasiasa, ambao hakuwataja, kwa kuchochea wachimbaji hao kutumia maandamano kudai haki wanazodai zimekiukwa kwa kunyimwa maeneo ya kuchimba madini.

Wachimbaji hao zaidi ya 3,000, awali waliandamana hadi katika ofisi ya kijiji hicho wakitaka kurudishiwa maeneo yao ya kuchimba dhahabu huku wakidai hawatambui uhalali wa leseni ya mwekezaji huyo.

Mmoja wa wachimbaji hao, Jackson Mwita, alisema walipewa agizo la siku saba la kuondoka maeneo hayo bila kufanyika maandalizi yoyote kuhusu hatima ya shughuli zao za kila siku za uchimbaji katika mgodi huo.

"Sisi tumezoea kuchimba madini maeneo hayo kila siku za maisha yetu. Tumesikitishwa na agizo la ofisa madini mkoa kututaka kuondoka ndani ya siku saba bila maandalizi yoyote. Hatujui tutakwenda wapi," alisema Mwita.

Ofisa Madini Mkoa wa Mara, Salim Msuya, alisema serikali imezuia shughuli za uchimbaji katika mgodi huo ili kuzuia uvunjifu wa amani na maafa zaidi kati ya wananchi na mwekezaji aliyemtaja kwa jina la John Bina.

Alisema serikali inaendelea kutatua mgogoro huo ikiwa ni pamoja na jitihada za kudhibiti utoroshaji madini nje ya wilaya na nje ya nchi, ili kuwezesha upatikanaji wa kodi halali ya serikali.




Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Bruce Mwile (wapili kushoto) na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Water.Org, Injinia Francis Musinguzi wakibadilishana mikataba ya ushirikiano katika hafla fupi iliyofanyika makao makuu ya Benki ya CRDB jijini Dar es Salaam jana. Wanaoshuhudia pichani ni wanasheria wa Benki ya CRDB na Shirika la Water.Org. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wahitimu wajiajiri kupitia ujuzi wao

**Na Joseph Mwendapole**

UTAFITI uliofanywa kuhusu wanafunzi wanaohitimu katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), umeonyesha kuwa asilimia kubwa wamekuwa wakijiajiri kwa kutumia ujuzi wao.

Hayo yalibainishwa jana Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Kamati ya Kufuatilia Maendeleo ya Wahitimu, Ambele Mtafya, alipowasilisha utafiti uliofanyika kuhusu wahitimu wa taasisi hiyo.

Alisema miezi sita baada ya kuhitimu, taasisi hiyo imekuwa ikifanya utafiti kujua wahitimu waliko na wanachofanya, kama wameajiriwa au wamejiajiri ili kujua kama mitaala iliyopo inakidhi mahitaji ya soko.

Mtafya alisema wamekuwa wakizungumza na waajiri wenyewe wanapotokea wahitimu wao kujua wanakuwa kwenye viwango gani na kwamba waajiri hao wanawapa mrejesho unaowasaidia kuboresha mafunzo ili kuendana na kinachohitajika kwenye soko la ajira.

"Tumeshazungumza na waajiri na wahitimu wetu sasa tunajadili tafiti ambazo tulizipata ili taasisi tujipange tunakwendaje mbele kuboresha mitaala yetu iweze kuendana na mahitaji ya teknolojia inayotumika kwenye uzalishaji viwandani," alisema.

Alisema wamekuwa wakiwapeleka wanafunzi wao kwenye viwanda kufanya kazi wakiwa masomoni ili kupata uzoefu unaowawezesha kufanya kazi kwa ufanisi baada ya kuhitimu.

Kaimu Mkurugenzi wa Taaluma wa DIT, Dk. Petro Pesha, alisema utafiti huo umewasaidia kutathmini umuhimu wa programu zao na kubadilika pale inapobidi ili waweze kukabiliana na mabadiliko ya dunia katika soko la ajira.

Alisema ina lengo la kuunga mkono ajenda ya serikali ya kuigeuza Tanzania kuwa ya uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

"Lengo letu linalazimu kuwepo kwa mfumo thabiti wa wataalamu wenye ujuzi wa hali ya juu waliofunzwa chini ya mfumo wa elimu na mafunzo unaozingatia umahiri yaani CBET, wenye vifaa si tu kufanya uvumbuzi bali kuongoza katika maendeleo ya kiteknolojia na tafiti za viwanda," alisema.

Alisema DIT ina jukumu kubwa katika kuendeleza uchumi wa taifa kwa kutoa wafanyakazi wenye ujuzi wa hali ya juu kwenye tasnia hiyo na kuongeza kuwa inasisitiza umuhimu wa ufuatiliaji wa mara kwa mara wa tathmini ya wahitimu wao ili kuhakikisha programu zao zinaendelea kuwa muhimu na zenye ufanisi.

"Katika mwaka wa masomo 2023/2024 DIT ilifanya utafiti wa kufuatilia wahitimu wa mwaka 2022 ili kutathmini athari za elimu yetu kwenye soko la ajira na kutathmini umuhimu wa programu yetu," alisema. Aliongeza kuwa utafiti huo ulilenga kuchunguza maeneo matatu muhimu moja likiwa ni umuhimu na ubora ambapo wamechunguza mitazamo ya wahitimu na waajiri wa mwaka 2022 kuhusiana na umuhimu wa mtaala na ubora wa ufundishaji.

Alitaja eneo jingine la masomo kuwa ni ajira ya wahitimu ambapo walichunguza mitazamo ya wahitimu wenyewe kuhusu ubora wa kazi, umuhimu wa elimu yao na ufanisi wa mafunzo yao katika kupata ajira. Dk. Pesha alitaja eneo lingine la utafiti kuwa ni kuridhika kwa waajiri ambapo walichunguza mtazamo wa waajiri kuhusu ubora wa wafanyakazi walioajiriwa kutoka kwa wahitimu wa taasisi hiyo.

Alisema matokeo ya utafiti yatatoa ufahamu muhimu kuhusu hali ya sasa ya wahitimu wa DIT kuunganishwa katika soko la ajira na ufanisi wa programu ya taasisi na maeneo ambayo wanaweza kufanya uboreshaji.

Alisema kuwa wamekuwa wakifanya utafiti wa mitaala kabla ya kuanza kuitumia na kuongeza kuwa jambo hilo limesaidia kuzalisha wahitimu wenye sifa katika soko la ajira kwani tafiti walizofanya zimeonyesha hivyo.

## Othman ataka mifumo imara ya biashara

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amehimiza umuhimu wa kuwapo mfumo wa biashara unaotoa unafuu kwa wawekezaji ili kusaidia jitihada za kukuza uchumi.

Othman aliyasema hayo jana Mbweni, mjini Unguja katika mahojiano maalum na kituo cha Clouds FM, akielezea masuala mbalimbali yahusuyo Zanzibar.

Alisema uchumi wa Zanzibar unategemea zaidi shughuli za huduma, tofauti na wa Tanzania Bara ambao unaendeshwa kwa rasilimali na maliasili zilizoko na kwamba mfumo wake kiuchumi, yakiwamo masuala ya kodi, unapaswa kuwa tafauti na Zanzibar.

Alitaja masuala kama vile kodi, taratibu na sheria za uwekezaji ikiwamo usajili wa vitegauchumi na kampuni, vibali vya biashara na mambo kadhaa kuwa ni masuala yanayotakiwa kufanyiwa mageuzi kwa upande wa Zanzibar, ili kupatikana kwa wepesi na unafuu kuliko ilivyo sasa.

Alisema hatua hizo ni muhimu katika jitihada za kuiwezesha Zanzibar kuwa na faida zaidi ya kiuchumi kama zilivyofanya nchi zingine duniani katika kuleta mageuzi yenye tija katika uwekezaji na kuleta maendeleo.

Pia alisema katika hatua hizo pia kunahitajika mageuzi makubwa katika upatikanaji wa rasilimali watu kwenye maeneo tofauti ya wataalamu watakaoiwezesha Zanzibar kupiga hatua za haraka kiuchumi na kukuza maendeleo katika nyanja mbalimbali.

Othman alisema jitihada hizo pia zitawezesha fursa nyingi za kiuchumi na kimaendeleo Zanzibar kutumika vyema na kutimiza matarajio kwenye mafanikio ya kiuchumi na kuchangia kukuza maendeleo haraka.

Kuhusu kupambana na umaskini, Othman alisema viongozi wengi wa Tanzania wametoka katika familia na maisha ya umasikini na kwamba wanayatambua vilivyo matatizo waliyoxnayo wananchi na kupata kwao nafasi za uongozi wanapaswa kuzitumia kama fursa za kuleta kasi ya maendeleo badala ya kubweteka na vyeo walivyo navyo.

Alisema viongozi wa Tanzania wanapaswa kutojijenga zaidi katika msingi ya kisiasa na badala yake jitihada na maarifa yao wayaelekeze kusaidia kukuza misingi ya kiuchumi kwa kuzitumia vilivyo rasilimali zilizopoili kuleta maendeleo ya wananchi.

Akizungumzia maadili kwa viongozi wa umma Zanzibar, makamu huyo qwa kwanza wa Rais alisema sheria iliyopo ina mambo na miongozo mingi mizuri, lakini Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma inahitaji kuwa na meno zaidi ikiwamo kujitegemea kifedha na kimamlaka ili ifanye kazi kwa ufanisi tofauti na ilivyo sasa.

Kuhusu suala la Serikali ya Umoja wa Kitaifa, Othuman alisema hatua hiyo inalenga kuwapo mazingira sahihi ya kutengeneza mfumo na sera sahihi ili kuiwezesha Zanzibar kuwa na mazingira bora ya kisiasa ya kuondokana na mivutano.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Suala la rushwa miungu watu utumishi umma lifikie tamati*

**UTUMISHI** wa umma ni kuwatumikia watu. Huu ni msemo ambao umekuwapo enzi na enzi katika utumishi wa umma ukimaanisha kwamba mtu anapoingia katika kada hiyo, wajibu wake mkubwa ni kutoa huduma kwa wananchi kulingana na eneo alilopangwa kufanya kazi.

Tangu serikali ya awamu ya kwanza, ilisisitizwa kuwa watumishi wa umma katika ngazi zote, wajibu wao ni kuwatumikia wananchi kwa maana ya kuwahudumia wanapofika kwa ajili ya jambo fulani kwenye ofisi hizo. Kama ni ardhi, mteja anapaswa kusikilizwa shida yake na kutatuliwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu. Na kama kuna migogoro ya ardhi, maofisa wanaohusika na sekta hiyo wanatakiwa kuchukua hatua na kuitatua.

Kutokana na dhima hiyo, aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Hawa Ghasia, aliwahi kusema utumishi wa umma umefanywa kichaka cha baadhi ya watu kuijinufaisha badala ya kuwahudumia wananchi.

Ghasia alisema baadhi ya watumishi wa umma wamegeuka kuwa miungu watu kwa kuendekeza rushwa hivyo kuwafanya wananchi kuamini kwamba bila kutoa chochote kwa ofisa anayehusika kutoa huduma hiyo hawezi kuhudumiwa. Hakuishia hapo bali alisema neno 'njoo kesho' limekuwa msamiati maarufu katika maeneo mbalimbhali ya utumishi wa umma kwa kuwataka wananchi kurudi siku inayofuata wanapotaka huduma, sababu kubwa ikiwa kutengeneza mazingira ya rushwa.

Hali hiyo hiyo hivi sasa imeota mizizi kuanzia ngazi ya serikali za mitaa. Mtu anapokwenda kuomba barua ya utambulisho kwa mjumbe anaombwa kutoa kati ya Sh. 2,000 na 5,000 kwa kile kinachoelezwa kuchangia gharama za viandikia. Anapofika pia ofisi ya serikali ya mtaa, anatakiwa kutoa chochote ili kupata huduma stahiki.

Kuwapo kwa vitendo vya rushwa na miungu watu katika utumishi wa umma kumekuwa kukijidhihirisha kila mwaka wakati Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) inapotoa taarifa za taasisi za umma zinazolalamikiwa kukithiri kwa vitendo vya rushwa. Miongoni mwa taasisi ambazo kila mwaka zimekuwa zikitajwa kuongoza kwa vitendo hivyo ni polisi, mahakama, serikali za mitaa, ardhi na afya.

Juzi, Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo, alikutana na wenyeviti wa bodi na wakuu wa taasisi zilizo chini ya wizara yake na kukemea wale wanaojifanya miungu watu na kuwataka wabadilike katika utendaji wa kazi zao za kila siku. Alisisitiza kuwa jambo la kwanza katika wizara hiyo na taasisi zake ni kutoa huduma kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu na kuifanya wizara kuwa ya mfano katika utoaji huduma na kuchangia pato la taifa.


Pamoja na kwamba Waziri Jafo amerejea kauli hiyo, jambo la watumishi wa umma kuendekeza rushwa na umangimeza huku baadhi wakijiona miungu watu na bila kutoa huduma lazima wasujudiwe na kuwapa chochote, ni la kawaida na limekuwa kama kanuni ndani ya serikali.

Mfano halisi ni malalamiko ya wastaafu kucheleweshewa mafao yao katika mifuko ya hifadhi ya jamii. Kila wanapokwenda kufuatilia mafao yao baada ya kukoma kwa utumishi wao, wanazungushwa na kupewa kauli kuwa baadhi ya nyaraka zinakosekana, mradi watoe chochote ili wahuduniwe. Kwa ujumla jambo hili limekuwa sawa na donda ndugu huku likionekana kukosa dawa mahsusi.

Kama ni kusemwa, jambo hili limezungumzwa sana na viongozi wa serikali katika awamu zote tangu kupatikana kwa uhuru wa nchi, hivyo kuwa sawa na ngoma iliyopigwa sana na mwisho inakaribia kupasuka.

Ni vyema sasa hatua zikachukuliwa kwa vitendo badala ya kusemwa majukwaani huku wananchi wakiendelea kuteseka na hata kutoa rushwa au kuwatumia viongozi kwa sababu ya kujuana ili kupata huduma zinazostahili. Wakati wa vitendo ni sasa ili kutokomeza rushwa, umangimeza na miungu watu katika utumishi wa umma.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



## *Serikali ije na chanzo, ufumbuzi wa kudumu moto kwenye masoko*

Na Adam Fungamwango

**KWA** miaka ya hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la masoko kuungua nchini. Imekuwa ikitokea kila mara na kusababisha madhara na hasara kubwa kwa wafanyabiashara na wateja wao.

Ufunguaji wa masoko haya umeendelea kulitesa taifa, kwani masoko yote mashuhuri nchini yameshapitia kadhia hii, likiwamo Soko Kuu la Kariakoo, Dar es Salama.

Kila madhara haya yakitokea timu ya uchunguzi huundwa ili kubaini tatizo na mara nyingi kinachobainika mara nyingi kinafanana kwa kiasi kikubwa, tofauti yake ni mazingira tu.

Mara nyingi chanzo huo ni mshumaa, mama lishe kusahau alichokiacha kwenye jiko la mkaa, kama supu, maharage, au vingine vinavyofanana na hivyo.

Kingine ni shoti ya umeme, hivyo vyote vinatajwa kuwa ni vyanzo vya moto kwenye masoko mbalimbali nchini.

Cha kushukuru ni kwamba huwa hakuna vifo wakati wa masoko yakiungua, na sababu kubwa mara nyingi huungua usiku kipindi ambacho hakuna watu, wafanyabiashara wameshafunga biashara zao.

Kwa sasa hatujui ni wapi tena kunafuata, kwa sababu matukio hayo wamekuwa mengi kiasi kwamba kama vile hata wananchi wameshaanza kuyazoea.

Ambao wanahuzunishwa ni wale waliopata hasara, hasa wafanyabiashara, wateja wao, ndugu jamaa, marafiki, na hata watu wa eneo hilo, lakini wengi wameonekana kama kuyazoea.

Ndiyo maana hata soko likiungua, mtu akiangalia kwenye mtandao wake wa kijamii, au akisikia kwenye vyombo vya habari, anaona kama vile huenda ni marudio ya masoko yalioungua huko nyuma, na si mapya.

Ifike wakati sasa litafutwe suluhisho la kudumu kuhusu kuungua kwa masoko kwa sababu kunasababisha athari kubwa, ikiwamo kuwarudisha watu kwenye umasikini, na serikali inakosa kodi.

Kuna watu wameshanunua bidhaa, pesa yote wameshaiweka kwenye mzigo, wana madeni ya mikopo sehemu mbalimbali, lakini moto unakuja na kuwatia umasikini ndani ya dakika 20 tu.

Tume zimeundwa na kuundwa, lakini bado halijawa suluhisho. Sana sana zinakuja kujulisha umma tu chanzo chake ni nini.

Mimi nadhani imefikia wakati wateuliwe wataalam, ambao watafanya kazi ya kufanya uchunguzi yakinifu ya sababu kuu ya masoko mengi kushika moto.

Na kwa nini huwa hayaungui mchana wakati wa jua kali, badala yake usiku, hasa wa manane? Hawa waende mbali zaidi na kutafuta suluhisho la kufanya ili matukio haya wasijirudie tena. Itakuwa haina maana kujua chanzo tu, halafu tahadhari haichukuliwi.

Ni sawa na mtu anayeumwa malaria, anakwenda hospitali kupima, akiambiwa ugonjwa anaoumwa, basi anaondoka bila kupata dawa, yaani yeye alichokuwa akitaka ni kufahamu tu anaumwa nini. Huyu malaria itamuua.

Kama ni kubadilisha nyaya za umeme, basi zibadilishwe kwenye masoko yote, kama ni mama lishe, basi waambie supu au maharage yao wapikie majumbani, au nje ya soko, na waingie ndani wakiwa tayari vyakula vya vimeshaiva.

Kama kuna kingine ambacho kitagundulika kuna ni sababu utengenezwe mpango mkakati wa kuondoa vyanzo vyote vinavyosababisha au viashiria vyake.

Nadhani hapa ndipo masoko yetu yatapoanza kuwa salama, lakini tuache tu tume ziwe na kazi tu ya kutaja chanzo halafu imeisha, wafanyabiashara wetu wataendelea kulia kila kukicha na serikali kushindwa kupata mapato yake kwenye kodi na hata Halmashauri kukusanya ushuru.

HABARI KITAIFA

# Marekani, India kuongeza nguvu uzalishaji nishati mbadala nchini

**Na Waandishi Wetu**

KILIO cha Tanzania kufikia adhima ya kutumia nishati safi, huenda kikazaa matunda baada ya Serikali ya Marekani na India, kuungana kukuza na kuimarisha miundombinu ya nishati hiyo nchini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Ubalozi wa Marekani nchini muungano huo ni wa kwanza katika bara ya Afrika na unatekelezwa na shirika lisilo la kiserikali la Marekani 'The Asia Foundation'.

Taarifa hiyo ilisema, muungano huo utaboresha uwezo wa kila nchi na kufanya gridi ya taifa kuwa na nguvu zaidi, mifumo ya udhibiti na sera iliyoboreshwa na muungano wa kikanda imara, pamoja na kuendeleza matumizi ya nishati ya jua nchini.

Taarifa hiyo iliongeza kuwa Marekani itaendelea kuwa mshirika mkubwa wa Tanzania katika kuharakisha usambazaji wa umeme ili jamii ziweze kupata nishati safi na ya uhakika.

"Tangu mwaka 2013, mpango wa USAID wa Power Afrika ulipoanza, Tanzania imepata mafanikio makubwa katika sekta ya nishati kwa kuongeza upatikanaji wa umeme kutoka takribani watu milioni 1.2 hadi zaidi ya watu milioni 4.5 mwaka 2023.

"Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) linashirikiana na Vituo vya Ubora vya India, vikiwamo Grid Controller of India Limited na NTPC School of Business, kuwashirikisha watunga sera, wadhibiti, watoa huduma, wasomi na sekta binafsi nchini Tanzania ili kupanua wigo wa matumizi ya nishati mbadala na kukuza uwekezaji wa nishati inayozingatia tabianchi," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Kaimu Mkurugenzi Mkazi wa USAID Tanzania, Alexander Klaits, alisema: "Sasa tunaanza ushirikiano mpya muhimu, pamoja na serikali ya India, unaopanua ushirikiano wa nishati na Tanzania" ilinukuu sehemu ya taarifa hiyo Ushirikiano huo utaimarisha uwezo wa ndani, na kuongeza fursa za biashara baina ya kampuni ya Marekani nchini Tanzania.

"Tunayo heshima kushirikiana na serikali ya India kusaidia Tanzania kuendelea kuwa msafirishaji mkuu wa nishati katika kanda ya Afrika Mashariki," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Balozi Mdogo wa Ubalozi wa India, Manoj Verma, alisema ni jambo la kujivunia kuona ushirikiano wa kwanza kati ya India na Marekani katika bara la Afrika unafanyika nchini.

Katika taarifa hiyo alisema ushirikiano huo unatoa mfano imara wa kimkakati kati ya Tanzania na India, kwa kuzingatia maendeleo ya nishati mbadala na usimamizi wa gridi ya taifa, na kwamba ushirikiano huo utaongeza juhudi za Tanzania inapokaribia kukamilisha miradi mikuu ya nishati na kuunganisha gridi yake na nchi katika ukanda huu.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dk. James Mataragio, katika taarifa hiyo alisema Tanzania itafaidika kutoka na uzoefu waliona nchi hizo katika kutengeza nishati ya jua na upepo. Kamishna Msaidizi wa Nishati Jadidifu kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Imani Mruma alisema kwa sasa Tanzania inazalisha megawati 10.5 za umeme ulioounganishwa katika gridi ya Taifa, unaotokana na masalia ya mimea kutoka kwenye Kiwanda cha Sukari cha Moshi TPC, na TANWART mkoani Njombe. Alitaja miradi inayotekelezwa kuwa ni umeme wa jua katika wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga unatekelezwa kwa awamu mbili, ya kwanza utazalisha megawati 50 ya pili itazalisha megawati 100.

"Kukamilisha kwa mradi huu itakuwa ni historia kwa nchi katika matumizi ya nishati jadidifu kuingiza kwenye gridi ya Taifa hata hivyo kuna miradi mingine ukiwemo wa joto ardhi eneo la Kyejo Mbaka wilayani Rungwe na Songwe ambapo wanatarajia kuzalisha megawati 200," alisema Mhandisi Mruma.

Aliongeza kuwa Wizara ya Nishati ipo kwenye hatua za maandalizi na upembuzi yakinifu kwa ajili ya kutekeleza mradi wa nishati ya upepo kwa mikoa ya Shinyanga, Singida Dodoma, Kilimanjaro, Iringa na Njombe ili ifikapo mwaka 2028 izalishe megawati 843.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dk. James Mataragio, alisema mpango wa serikali ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2034 zaidi ya asilimia 80 ya wananchi wawe wanatumia nishati safi ya kupikia.

Alisema Tanzania itafaidika na uzoefu na mafunzo ya Marekani na India katika kutengeneza nishati ya jua na upepo kwa ajili ya kuchochea maendeleo ya nishati mbadala na gridi ya taifa yenye nguvu zaidi nchini.

"Juhudi za ushirikiano kama hizi ni muhimu katika kushughulikia vikwazo vinavyotokana na nishati zinazokabili Taifa letu kwa kutumia utaalamu na rasilimali kutoka kwa washirika wa kimataifa, tupo kwenye njia nzuri ya kupiga hatua kubwa katika maendeleo endelevu ya nishati, kuboresha miundombinu na kujenga uwezo wa wahandisi wetu wa ndani kupitia mafunzo ya juu na kujifunza mbinu bunifu," alisema Mataragio.



Kifaa cha kuhifadhia taka-taka katika kituo cha daladala cha Tabata Segerea, jijini Dar es Salaam, kimenaswa na kamera yetu jana, kikiwa kimechakaa na kuhitaji ukarabati. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Kula kupindukia, kutokula muda mrefu kikwazo afya yako

**Na Christina Mwakangale**

KULA kupindukia, kutokula muda mrefu na kutozingatia lishe, kunaathari katika mwili wa binadamu.

Bingwa wa Upasuaji na Mkuu wa Idara ya Upasuji Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) Mloganzila, Dk. Eric Muhumba, amesema wanaokaa muda mrefu bila kula, wamo hatarini kupata vidonda vya tumbo (ulcers).

Kadhalika, watu wanaokula mlo kupitiliza bila kuzingatia lishe, wamo hatarini kuingia kwenye kundi la walio na unene uliopindukia (obesity).

Unene uliopindukia kitaalamu hutokea wakati fahirisi ya uzito wa mwili (Body index) wa mtu ni 30 au zaidi.

Dk. Muhumba aliiambia Nipashe kwenye Maonyesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF), yaliyohitimishwa rasmi Julai 13, mwaka huu na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi.

"Kundi la watu wanaoshinda njaa muda mrefu, wamo hatarini kupata vidonda vya tumbo, kutokana na acid (tindikali) iliyomo tumboni.

"Sababu kuu ya vidonda vya tumbo ni acid nyingi tumboni ambayo unaizalisha wewe mwenyewe. Pili ni kuwa na maambukizi ya bakteria wanaoitwa Helicobacter pylori (H. Pylori)," alisema bingwa huyo.

Pia, alisema hatari ya acid inayozalishwa kwa wingi tumboni hutokana na mtu kutokula muda mrefu, kula vyakula vinavyozalisha kemikali hiyo pamoja na msongo wa mawazo, huweza kusababisha utumbo kutoboka na kuhitajika upasuaji wa dharura.

"Kukaa na njaa muda mrefu, inasababisha acid inakuwa yenyewe tumboni inaanza kula kuta za tumbo.

Kuhusu matibabu ya ugonjwa huo, anasema huwa yanatatiza ndio sababu ya wengi wenye tatizo hilo, kuishi na ugonjwa muda mrefu.

"Matibabu yake kama ni maambukizi tutapima kwa kutumia endoskopi au kuchukua sehemu ya nyama eneo hilo, kama ni H.pylori yumo ataanza matibabu.

"Pili kama tatizo linasababishwa na acid kwa kutumia dawa. Kutibu vidonda vya tumbo ngumu sana. Unatakiwa kufuata masharti, usipovotibu vizuri tumbo linatoboka na itasabisha uchafu au chakula kusambaa maeneo yote, itahitajika upasuaji wa haraka.

"Upasuaji ni wa kuziba kile kidonda, ila wakati mwingine vidonda huwa vinavuja damu mtu akatapika damu. Lakini kingine katika mlango wa kutokea chakula kutoka katika tumbo la chakula, huweza kuziba.

"Pakiziba na kuweka kovu itasabaisha chakula kisiingie kwenye utumbo mdogo, mtu anakonda, anadhoofika kwa sababu chakula hakisafiri kwenda kwingine kujenga mwili," alisema bingwa huyo.

Dk. Muhumba akizungumzia wanaokula mlo kupindukia na kuwasababishia unene kupitiliza, tiba mojawapo ni kuwawekea puto tumboni ambalo husababisha mtu kula kidogo.

Alisema hadi sasa waliokwishawekewa puto tumboni MNH ni takribani 180 na matibabu hayo huwasaidia kupunguza hatari za Magonjwa Yasiyoambukiza (NCDs), kama vile presha na kisukari.

"Puto baadaye litatolewa baada ya mwaka mmoja. Inabidi wewe mwenyewe ujizoeshe kula kwa wastani ili usirudi katika uzito mkubwa, ambao kiafya ni hatari," alisema Dk. Muhumba.

Mtaalamu wa Lishe kutoka hospitali hiyo, Abubakar Abushiri ana ushauri kwamba jamii izingatie mlo kamili, bila kukosa mboga za majani zinazopikwa kwa wastani bila kusahahu kuweka mafuta kiasi, ili kuimarisha vitamini zilizomo katika mboga hizo.

"Mlo wa vyakula vyenye wanga mwingi ni tatizo, mfano wali, ugali wa unga uliokobolewa. Pima chakula kulingana na ushauri, sio lazima ujaze sahani kubwa yenye nyama nyekundu nyingi. Vyakula vyote ni muhimu mwilini, ila viwe na wastani. Uzito lazima uwiane na urefu wako," alisema Abushiri.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed






Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Prof. Elifas Bisanda (wa tatu kushoto) na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo hicho (Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaaluma), Prof. Alex Makulilo (wa tatu kulia), wakizindua nembo ya maadhimisho ya miaka 30 tangu kunzishwa kwa chuo hicho, jijini Dar as Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mavunde: Leseni 45 za utafiti madini zimerejeshwa serikalini

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI wa Madini, Anthony Mavunde amesema serikali imefuta na kuzirejesha leseni 45 za utafiti kati ya 102 zilizopo mkoani Rukwa, baada ya wahusika kushindwa kukidhi masharti.

Hayo yalibainishwa jana wakati wa kikao kilichofanyika kati ya kiongozi huyo na wadau wa sekta ya madini, baada ya uongozi wa wachimbaji wilayani Sumbawanga mkoani Rukwa kutoa ombi la kuongezewa eneo kwa ajili ya kuendesha shughuli za uchimbaji.

Alisema wamerejesha leseni hizo ili kutoa fursa kwa serikali kuyapanga vyema maeneo hayo kwa kutenga leseni kwa ajili ya wachimbaji wadogo na wawekezaji wakubwa walio tayari kuwekeza kwenye sekta ya madini.

"Rais Samia Suluhu Hassan ametupa maelekezo bayana ya kuhakikisha leseni zinatolewa zinafanya kazi na watu wasihodhi maeneo makubwa bila kuyafanyia kazi, ili kuchochea shughuli za uchimbaji na ukuaji wa sekta ya madini.

"Leseni hizi 45 zilikuwa zimeshikilia eneo kubwa la ekari 812,383 ambalo ni kubwa kuliko wilaya nzima ya Sumbawanga yenye ukubwa wa ekari 667,641.

Uchimbaji hapa mkoani Rukwa uko chini, hivyo ni jukumu la ofisi ya ofisa madini mkoa kuhakikisha mnachochea shughuli za uchimbaji," alisema Mavunde.

Ofisa Madini wa Mkoa wa Rukwa, Mhandisi Joseph Kumburu alimhakikishia Waziri Mavunde kusimamia utekelezaji wa maagizo hayo hasa katika kuchochea shughuli za uchimbaji kwakuwa mkoa huo umejaaliwa madini mengi ya aina tofauti na kwamba wana fursa kubwa ya kufanya vizuri.

Akiwasilisha taarifa ya wachimbaji, Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji mkoani humo (RUREMA), Masie Mwambegele aliomba serikali kuwapatia maeneo wachimbaji wadogo katika sehemu ambayo haifanyiwi kazi.

"Pia tunaiomba serikali iongeze nguvu kwenye eneo la utafiti ili wachimbaji wasichimbe kwa kubahatisha kama ilivyo sasa," alisema Mwambegele.

# Waziri akemea urasimu taarifa watumishi waliohama

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, ameagiza ifikapo Agosti 15, mwaka huu, taarifa zote za watumishi waliohama maeneo yao ya kazi ziwe zimehamishiwa walikohamia.

Amesema kuna usumbufu mkubwa wanaopata watumishi wa umma waliohama kutoka kituo kimoja kwenda kingine, huku akisema jukumu la kutafuta taarifa ni la mwajiri na si mwajiriwa.

Simbachawene alisema, kwa ambao hawatatekeleza agizo hilo hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa kwa wote watakaoshindwa kutekeleza jukumu hilo.

Pia, amepiga marufuku watumishi wa umma kusumbuliwa kufuatilia taarifa zao za kiutumishi wanapohamia kwenye kituo kipya cha kazi badala yake wafanye kazi zao, kwa kuwa hilo sio jukumu lao bali ni wajibu wa waajiri.

Simbachawene alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na watumishi na wananchi kwenye mkutano wa hadhara katika Kijiji cha Mlimo, Kata ya Lufu, Jimbo la Kibakwe, Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, jijini Dodoma.

Alisema suala la taarifa za mtumishi ni jukumu la mwajiri na kitendo cha taarifa za watumishi kutohamishwa kimesababisha watumishi hao kushindwa kupimwa kwenye mfumo wa e-tendaji kazi kwa vile kunakuwa hakuna taarifa za watumishi hao katika kituo kipya cha kazi.

Alisema watumishi wengi husumbuliwa kufuatilia taarifa zao walikotoka jambo linalopoteza muda mwingi wa uzalishaji.

Waziri Simbachawene alimwelekeza Katibu Mkuu- Utumishi kushirikiana na mamlaka zingine zilikokasimiwa madaraka hayo ya kuhamisha watumishi kuhakikisha mtumishi anapohama kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine asisumbuliwe kuhusu taarifa hizo. Alisema suala la kuhamisha taarifa za mtumishi kutoka alikokuwa na kwenda kituo kipya cha kazi ni jukumu la mkurugenzi au anayeongoza taasisi wakishirikiana na maofisa utumishi na kuongeza kuwa wanatakiwa kuhakikisha taarifa hizo zinahamishwa ndani ya mwezi mmoja ili watumishi waliohamishwa waendelee kufanya kazi zao kwa ufasaha.

"Utapimaje utendaji kazi wa mtumishi au kumpatia ruhusa mtumishi aliyepata dharula ilhali taarifa zake zipo sehemu nyingine, hii sio sawa, huko ni kuwatesa watumishi," alihoji Simbachawene.

Alisema malalamiko ya kutohamishwa kwa taarifa za watumishi yamekuwa mengi kutoka kwa watumishi huku akiwataka watumishi wanapohama kutekeleza majukumu yao na hakuna atakayesumbuliwa.

# Khoja Shia yaadhimisha siku ya Ashura kudumisha amani

**Na Mwandishi Wetu**

JUMUIYA ya Khoja Shia nchini yaadhimisha siku Ashura kwa kufanya matembezi ya Amani jijini Dar es Salaam, kama njia mojawapo ya kufikisha ujumbe kwa jamii ya kudumisha haki na amani katika kuenzi Msiba wa Imamu Hussain (a) Mjukuu wa Mtume Muhammad (S.A.W) aliuawawa huko Karbala nchini Iraq mwaka 61 A.H miaka 1400 iliyopita.

Matembezi hayo hufanyika kila mwaka na mwaka huu yalibeba ujumbe wa kudumisha haki na amani kama kumbukumbu ya kuadhimisha msiba wa Karbala uliotokea mwaka 61 A.H, katika tukio hilo la huzuni liliwaleta pamoja washirika kutoka kote.

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Muhammedrazza Dewji, alisema kufanyika kwa matembezi hayo jijini Dar es Salaam ni kuheshimu kumbukumbu ya Imam Hussain (as) na wafuasi wake 72, ambao walijitoa mhanga ili kulinda kanuni za haki, huruma, na uadilifu.

Alisema kuwa matembezi hayo yaliyoanzia na kumalizikia kwenye Msikiti wa Shia, jijini Dar es Salaam, yaliongozwa na Quran Tukufu, ikionyesha kujitolea kwa washiriki kwa maadili aliyosimamia Imam Hussain.

"Siku ya Ashura ina umuhimu mkubwa kwa Waislamu kote duniani, kwani inaadhimisha kifo cha shahidi cha Imam Hussain (PBUH), mjukuu mpendwa wa Mtume Muhammad (PBUH). Msiba wa Karbala ni ukumbusho wa kudumu wa umuhimu wa kusimama dhidi ya dhuluma, uonevu na ukosefu wa haki," alisema Mohammedrazza.

Alisema kuenzi kufanyika kwa matembezi hayo inaashiria kudumisha maadili katika ulimwengu na kuamrisha mema na kukataza maovu, kanuni ambazo zinavuka mipaka ya dini na tamaduni.

Pia alisema kuwa umuhimu wa msiba wa Karbala katika maisha ya leo sio tu tukio la kihistoria bali masomo yake yana umuhimu mkubwa katika ulimwengu wa leo.

Aidha, alisema kuwa msimamo wa Imam Hussain dhidi ya utawala dhalimu na wa ukandamizaji unasisitiza umuhimu wa uadilifu, haki na ushujaa wa kimaadili.

Vilevile, Mzee Mohammedrazza alisema kuwa katika wakati ambapo ukosefu wa haki na dhuluma bado vinaweza kupatikana, kujitolea kwake bila kuyumba kwa ukweli na uadilifu kunatoa mwanga wa matumaini na mwito wa kuchukua hatua.

"Masomo ya Maisha kutoka Karbala Hadithi ya Karbala inatufundisha masomo kadhaa madogo, lakini yenye nguvu ambayo yanaweza kutekelezwa kwa kuboresha sisi wenyewe, majirani zetu, jamii zetu, na nchi yetu," alisema Mohammedrazza.

Alizitaja baadhi ya masomo hayo madogo kuwa ni, kusimama kwa haki: "Kama Imam Hussain, tunapaswa kusimama dhidi ya dhuluma na ukandamizaji. Hili linaweza kutekelezwa kwa kutetea haki za wengine na kuhakikisha haki katika maingiliano yetu ya kila siku."

Mzee Mohammed razza alisema kuwa kupitia tukio hilo, Jumuiya ya Khoja Shia ililenga kusambaza maadili haya kwa Watanzania wenzao, ikionyesha umuhimu wa ujumbe wa Imam Hussain katika ulimwengu wa leo. Kwa kuadhimisha Ashura, Jumuiya inatumaini kuwahamasisha wengine kudumisha haki, huruma, na uadilifu katika maisha yao.





# Wabakaji watoto watupwa jela maisha

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

JESHI la Polisi mkoani hapa limetamba kushinda kesi 20 za ubakaji na kulawiti watoto huku washtakiwa wakifungwa miaka 30 na maisha jela baada ya kutiwa hatiani na mahakama.

Hayo yalisemwa juzi na kamanda wake, George Katabazi wakati akizungumza na NIPASHE kuhusiana na matukio ya ukatili dhidi ya watoto mkoani hapa kwa kipindi cha kuanzia Januari hadi Julai mwaka huu yaliyotokea mkoani hapa.

Katabazi, alisema kesi hizo walishinda baada ya kuwafikisha watuhumiwa 20 mahakamani na kufunguliwa mashtaka na kupatikana na hatia ya kubaka na kulawiti watoto hao wenye umri wa kuanzia miaka minne kwa nyakati tofauti.

Alisema kati ya hao, washtakiwa saba walipatikana na hatia kuhukumiwa kifungo cha maisha jela na wengine 13 miaka 30 kila mmoja.

Katabazi, alisema baada ya jeshi hilo kufanya uchunguzi, limebaini kuwa matukio hayo mkoani hapa yanasababishwa na imani potofu na ulevi wa kupindukia.

Kamanda huyo alisisitiza kuwa jeshi hilo litaendelea kuwakamata watuhumiwa na kuwafikisha mahakamani ili hatua kali zichukuliwe dhidi yao na kuwa fundisho kwa wengine wenye tabia kama hizo na kutokomeza vitendo hivyo mkoani hapa.

Mkazi wa Wilaya ya Babati, Amina Ramadhani wa Babati, akizungumza na NIPASHE kuhusiana na matukio hayo, aliiomba serikali kubadili sheria ili watuhumiwa wa ubakaji na ulawiti wasipewe dhamana.

Amina alifafanua kuwa ametoa ombi hilo baada ya kubaini kuwa wengi wa watuhumiwa hao, wakipewa dhamana wanakwenda kujadiliana na familia za watoto waliofanyiwa vitendo hivyo na kumalizana kienyeji.

Mkazi wa Mtaa wa Hangon Mathew Bayo, aliiomba serikali kuwapima akili watuhumiwa wa ubakaji na ulawiti watoto ili kubaini kama wana akili timamu au la.

Juni 26, mwaka huu, Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara, Dominick Mbwete akiongoza kikao cha tathimini ya utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya malezi makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto (PJT-MMMAM) ngazi ya mkoa, alisema kwa mujibu wa takwimu za hivi karibuni Manyara ni wa kwanza nchini kwa ukatili hususani wa watoto.

Mbwete aliwaomba wazazi na jamii kuchukua hatua ili kudhibiti ukatili unaoendelea mkoani hapa kwa watoto, kwa kuwalinda kwa kuwa ni wa taifa.

Mkuu wa Dawati la Jinsia la Polisi mkoani Manyara, Wilness Kimario kwenye kikao hicho aliwahakikishia wananchi kuwa dawati hilo liko tayari kuwakamata watuhumiwa kwa kuwa wana wapelelezi maalumu wanaofanya kazi kwa siri.



Mwenyekiti wa Umoja wa Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Babati Vijijini, mkoani Manyara, Emmanuel Khambay (wa pili kulia), akishika Mwenge wa Uhuru baada ya kuingia wilayani humo, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Usafishaji damu wanukia Mawenzi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro ya Mawenzi (MRRH), inatarajia kuanza kutoa huduma ya usafishaji damu (dialysis) ili kusogeza huduma kwa wagonjwa wanaohitaji huduma hiyo na kuwapunguzia gharama.

Serikali inataka kuongeza kiwango cha watu wanaofanyiwa dialysis kutoka asilimia 32 ya sasa hadi kufikia asilimia 50. Kaimu Mkuu wa Kurugenzi Upasuaji ya Mawenzi (MRRH), Dk. Zawadi Mahumbuga, alisema serikali ina mkakati wa kupanua huduma hizo mkoani Kilimanjaro wakati wowote kuanzia sasa.

"Tunategemea kutoa huduma za dialysis ambazo zitakuwa mashine 10 na vitanda vyake vitakavyotoa huduma kwa wakati mmoja.

"Tunatarajia kuanzisha huduma ya kusafisha damu kwa wagonjwa hapa hospitalini; tunaishukuru serikali kwa kutenga zaidi ya milioni 300, ambazo zitatumika katika ujenzi unaoendelea wa miundombinu ya kusafisha damu," alisema.

Awali akitoa taarifa kwa mbunge huyo, Kaimu Mkuu wa Kurugenzi ya Upasuaji ya MRRH, Dk Zawadi Mahumbuga, alisema wodi ya upasuaji yenye uwezo wa vitanda 22 ya wanaume iliyozinduliwa itasaidia kupunguza matatizo ya uhifadhi wa wagonjwa wanaotembelea kituo cha afya cha rufaa cha mkoa. "Hapa tunapokea takribani wagonjwa 60 kila mwezi, ambao wanahitaji matibabu ya upasuaji wengi wao ni wale wanaopata ajali, wodi hii mpya itasaidia kupunguza ongezeko la idadi ya watu, ingawa mahitaji ya wodi nyingi bado yapo," alisema.

Daktari Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk Edna-Joy Munisi, alisema kuwa maboresho ya wodi hiyo yataweka mazingira bora kwa watoa huduma na wapata huduma.

"Itajumuisha wagonjwa wote, wakiwemo wa mifupa, wa macho, kinywa na meno, pua, masikio na koo ambazo zote zitakuwa za kibingwa. Pia tunategemea kutoa huduma za afya ya dialysis ambazo zitakuwa mashine 10 na vitanda vyake vitakavyotoa huduma kwa wakati mmoja," alisema Dk. Munisi.

Aliishukuru serikali kwa kutenga zaidi ya Shilingi milioni 300 kwa ujenzi unaoendelea wa miundombinu kwenye idara ya huduma ya usafishaji damu hospitalini hapo.

Alitaja mengine yanayoendelea kufanyika katika hospitali hiyo kuwa ni pamoja na ujenzi wa kichomeo kipya cha kuteketeza vifaa hatari vinavyotumika hapo na vituo vya afya. Alisema kichomea hicho kipya kina uwezo wa kuteketeza kati ya kilo 180 na 200 za vifaa hatarishi kwa saa, ikilinganishwa na cha zamani kwa kilo 25 hadi 40 sawa na kilo moja.

# Wanufaika TASAF wajivunia mafanikio

**Na Restuta James,** MOSHI

BAADHI ya wanufaika wa ruzuku inayotolewa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), katika Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro wameanzisha miradi ya biashara, ufugaji wa kuku, njiwa na nguruwe.

Wanufaika hao ni wale wanaotoka kaya zilizokuwa kwenye ufukara wa kukosa chakula na huduma muhimu kama makazi na malazi.

Wakizungumza na waandishi wa habari waliowatembelea wakati wa ziara ya TASAF iliyolenga kuona maendeleo ya walengwa hao ambao ni miongoni mwa kaya 400,000 zitakazoondolewa kwenye ruzuku hiyo, walisema mfuko huo ni mkombozi wao kiuchumi.

Mkazi wa Mtaa wa Kariwa Chini, Kata ya Rau, Caroline Minja, alisema alijiunga na TASAF mwaka 2015 akiwa anaishi kwenye chumba kimoja cha udongo na watoto wake watatu; na kwamba ruzuku imemwezesha kununua mahitaji ya watoto na kujenga nyumba ya kuishi.

Caroline, alisema TASAF imempa mafunzo ya namna ya kutunza fedha, kuendesha biashara na kuikuza jambo lililomwezesha kufuga nguruwe, kuanzisha kilimo cha bustani na genge la kuuza bidhaa mbalimbali.

"Kama mnavyoona nimejenga nyumba ya vyumba viwili kwa matofali ya kuchoma, ina umeme na nimefanikiwa kuanzisha genge kwa ajili ya kipato cha kila siku. Nimejiunga pia na kikundi cha kuweka na kukopa ili niendelee na nidhamu ya kutunza fedha," alisema.

Elizabeth Shirima, alisema TASAF imemwezesha kukuza mradi wa ushonaji nguo kwa cherehani.

Mkazi wa Mtaa wa Sabasaba katika Kata ya Rau, Lucy Tenga, alisema mfuko huo umemwezesha kuanzisha mradi wa kufuga kuku wa nyama na kumwingizia kipato cha uhakika kila baada ya wiki nne.

"Watoto nao wamesoma na nimejifunza kuweka akiba. Ninachoweza kusema ni kwamba fedha kidogo inaweza kutupeleka mahali pazuri, kwa sababu ruzuku tuliyokuwa tunapewa haikuwa kubwa, lakini baada ya mafunzo kutoka kwa wataalamu tumejua kutumia na kuweka akiba walau kidogo," alisema.

Takwimu zinaonyesha asilimia nane ya Watanzania wanaishi kwenye umasikini uliokithiri kutokana na kukosa kipato cha kujikimu kimaisha na kuendesha familia.





# Uhaba wa madarasa waikumba Mwanza

**Na Vitus Audax,** MWANZA

HALMASHAURI ya Jiji la Mwanza linakabiliwa na upungufu wa madarasa 1,632 kwa shule za awali na msingi na kusababisha msongamano wa wanafunzi madarasani.

Hayo yamebainishwa na Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi wakati wa mkutano baina ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda, viongozi wa serikali, watumishi na wadau wa maendeleo wilayani humo.

Makilagi, alisema jiji hilo, pia linakabiliwa na upungufu wa matundu ya vyoo zaidi ya 3,807 na madawati 17,771 katika shule hizo.

Alisema wanaendelea kupanga mikakati ya kukabiliana na upungufu ili kuwaondolea adha wanafunzi katika shule hizo na kuinua kiwango cha ufaulu.

Kwa upande mwingine, mkuu huyo wa wilaya, alimuomba Mtanda kumaliza tatizo la uhaba wa maji katika maeneo ya Buhongwa, Lwanhima, Igoma na Butimba ili wakazi wake waanze kupata huduma hiyo ipasavyo.

Akizungumza katika kikao hicho, Mtanda alilitaka jiji hilo kutumia fedha za mapato ya ndani kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kusogeza huduma kwa wananchi.

Alisema kwa mujibu wa makusanyo ya fedha kwa mwaka wa fedha wa 2023/24 ulioishia Juni 30, mwaka huu, jiji hilo lilipaswa kupeleka Shilingi bilioni 10 kwenye miradi ya maendeleo.

Alisema badala yake lilipeleka Shilingi bilioni nane na kusalia Shilingi bilioni mbili.

Mkuu huyo wa mkoa, aliagiza kiasi hicho kilichobaki kielekezwe katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

"Ukitaka kujua mimi ni nani, chezea fedha za miradi, yaani mradi usipokamilika wakati fedha zipo ni lazima nikupeleke TAKUKURU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa)," alisema na kusisitiza kuwa: " Sitakuacha maana hauwatakii mema wananchi ambao wanasubiri huduma kutoka kwenye miradi inayotekelezwa."



Wachuuzi wa nyama choma wakiandaa kwaajili ya wateja wao katika eneo maarufu kwa kitoweo hicho kwa gharama nafuu, mjini Bariadi hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Sita kizimbani kwa kuiibia CRDB 300m/-

**Na Shaban Njia,** KAHAMA.

WATU sita wamefikishwa mahakamani kujibu mashtakta ya uhujumu uchumi na kuiba kiasi cha Shilingi milioni 305 katika Benki ya CRDB Tawi la Kahama mkoani Shinyanga.

Washtakiwa hao waliofikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kahama na kusomewa mashtaka hayo ni Carline Kazinza (43), Msafiri Yohana (44), Salumu Juma (46) Askari wa Jeshi la Wananchi (JWTZ), Mark Mgeta (41) na maofisa wa benki hiyo, Ally Habibu (40) na Rafiki Macha (27).

Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Jukaeli Jairo alidai kuwa washtakiwa hao walitenda kosa hilo Julai 4, mwaka huu katika benki hiyo.

Jairo alidai kuwa washtakiwa wawili ambao ni wafanyakazi wa benki hiyo wanadaiwa kushindwa kutumia utalaamu wao kuzuia wizi huo wa kiasi hicho cha fedha usifanyike.

Alidai mshtakiwa namba moja hadi nne, wanakabiliwa na makosa 11 kati ya 12, likiwemo kuunda genge la uharifu, kughushi nyaraka, kula njama na kutoa Sh.milioni 95 kwenye akaunti yenye jina la Mariam Faisali na kuhamisha kiasi cha Sh.milioni 180 bila kuwa na haki ya kisheria.

Alidai vilevile wanadaiwa kutoa Shilingi milioni 30 kutoka kwenye akaunti ya Mariam ya Faisali, kughushi Kitambulisho cha Taifa (NIDA) cha mteja huo na kukutwa na mali ya wizi kiasi cha Shilingi milioni 30 isivyo halali.

Aliiomba mahakama hiyo kumpatia siku 14 kukamilisha upelelezi wa mashtaka hayo na kuzuia dhamana kwa washtakiwa hao ili wasiharibu msingi wa kesi.

Alisema kwa mujibu wa sheria, shtaka namba moja ni la uhujumu uchumi na mahakama hiyo haina mamlaka kisheria ya kulisikiliza.

Wakili wa utetezi, Gervas Genea aliomba mahakama hiyo kuwapatia dhamana wateja wake na kupinga ombi la mwanasheria huyo wa serikali kwa madai ya kuharibu upelelezi wake.

Hakimu Mfawidhi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Edmund Kente, alikubaliana na ombi la mwanasheria huyo wa serikali na kuahirisha kesi hiyo hadi Julai 29, mwaka huu na kuamuru washtakiwa hao kurudishwa rumande baada ya kunyimwa dhamana.

# Makandarasi goigoi Shy wamkera RC

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga Anamringi Macha, ameonyesha kukerwa na makandarasi wasio na uwezo kupewa kazi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara na kukwamisha miradi ya maendeleo.

Akizungumza katika kikao cha Bodi ya Barabara, Macha alisema kuwa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), wamekuwa wakifanya kazi nzuri, lakini wanakabiliwa na kasoro ya usimamizi wa makandarasi.

"Jitafakalini katika hili mnapotoa kazi kwa makandarasi, msiwapatie kazi bila ya kujiridhisha uwezo wao na msiwapatie kazi wenye kazi nyingi wanashindwa kukamilisha kazi zao kwa wakati," alisema Macha.

Aliwataka wakuu wa wilaya kuendelea kuwachukulia hatua makandarasi wanaotekeleza miradi.

Macha, alikemea tabia ya baadhi ya wananchi kuharibu miundombinu ya barabara kwa kupitisha mifugo, kuiba alama za usalama barabarani, kuvunja taa, kufanya biashara kando ya barabara, na kudhibiti magari yenye uzito mkubwa.

Alionyesha kukerwa na Manispaa ya Kahama kwa kukithiri wa uchafu, chupa kutupwa kwenye mitaro ya barabara.

Alimuagiza mkurugenzi wa manispaa hiyo kuchukua hatua za haraka ili kuimarisha usafi na kuwachukulia hatua watu wanaochafua barabara.

"Kishapu kuna miradi ya barabara ya mwaka 2023/24 bado haijatekelezwa kabisa, na sasa tunakwenda kwenye mwaka mwingine wa fedha 2024/25 na baadhi ya makandarasi hawapo eneo la mradi sababu hawana uwezo na sijui walipewaje kazi?" alihoji Mbunge wa Kishapu, Boniphace Butondo.

Meneja wa TARURA Mkoa wa Shinyanga, Avith Theodory, alisema makandarasi wengi wamekuwa wakikuomba kazi wakiwa na sifa nzuri na wanapopata inagundulika kuwa uwezo wao ni mdogo na hawana mitaji.

Meneja wa TANROADS wa mkoa huo, Samwel Mwambungu, alisema kwa mwaka wa fedha 2023/24 walitengewa kiasi cha Shilingi bilioni10.6, lakini wakapokea Shilingi bilioni 5.5 hadi kufikia Juni 30.

Alisema kwa upande wa miradi ya kimkakati, ujenzi wa uwanja wa Ndege Ibadakuli katika eneo la kurukia ndege umefikia asilimia 70 na jengo la abiria asilimia 30.

Alisema barabara ya Kolandoto hadi Mhunze imetengewa Shilingi bilioni moja kuanza ujenzi kilomita 20 na ya Oldshinyanga hadi Solwa upembuzi yakinifu umekamilika.


Ukurasa 14

Kilio bei ya ufuta, ghafla kilivyogeuka tabasamu kwa wakulima Mkuranga




Sare za bodaboda na ufumbuzi wa ajali!

Ukurasa 13

BUFE
IJUMAA JULAI 19, 2024
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

### USHINDI BIASHARA KIMATAIFA...

# Rais azindua lami kilomita 107 hadi Bandari Kassanga, neema kwa mizigo

**Na Mwandishi Wetu**

JUZI Jumatano, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akahitimisha ziara yake iliyochukua siku saba mikoa ya Rukwa na Katavi na jana akakanyaga ardhi ya mkoani Songwe, kuanzia mji mdogo wa mpakani, Tunduma.

Huko Rukwa alikotoka, amewaachia zawadi kwa kuzindua barabara ya lami umbali kilomita 107. 14, kutoka Manispaa ya Sumbawanga - Matai hadi Bandari ya Kasanga, ambayo nayo imekarabatiwa kwa kina, kazi iliyokamilika miaka michache tu iliyopita.

Hiyo bandari nayo katika nafasi yake ni 'bidhaa mpya' mahali hapo ikihudumia mataifa jiorani kama Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) na Zambia, ikinufaisha uchumi wa nchi kwa ujumla.

Uzinduzi wa Rais, ukaambatana na rai yake kwa wananchi kuitunza barabara hiyo kwa manufaa ya kızazi kilichoko na kijacho, akinena:

"Kabla ya barabara hii kujengwa, nimeambiwa usafiri kuelekea bandarini ilikuwa inachukua hadi siku nzima, lakini baada ya barabara hii kujengwa, ni masaa mawili tu umefika Bandarini Kasanga."

Akaendelea: "Niwaombe Wananchi na Kalambo (wilaya) na wasafirishaji wote kutunza miundombinu ya barabara, kwa kuacha kulima au kufukua fukua pembezoni mwa barabara kwani kufanya hivyo, kunasababisha kuharibika kwa haraka barabara zetu."



Dk. Samia Suluhu Hassan, alipozindua Barabara ya Sumbawanga - Matai hadi Bandari Kasanga. **PICHA: MTANDAO.**

Akawafafanulia, kwamba ni barabara inayowarahisishia usafiri na usafirishaji wa mazao na mifugo kutoka mkoani Rukwa kwenda maeneo mingine ya nchi jJirani, kama Rwanda, DRC na Burundi.

"Tunaenda kukuza uchumi wa biashara kati yetu na nchi jirani na wananchi wa Kalambo (wilaya yenye Bandari Kassanga) ni wakulima wazuri sana.

"Sasa mtapata urahisi wa kusafirisha na sio Kalambo peke yake, mazao yatakayolimwa ndani ya mkoa wa Rukwa na Katavi yatapata urahisi wa kusafirishwa," anasema Dk. Samia.

Rais akawataka wakazi kutofanya shughuli za kijamii kama kilimo na kuchimba pembezoni mwa barabara, nao wakimhakikishia watalinda miundombinu hiyo inayojengwa na serikali.

"Ujenzi wa barabara ni gharama sana. Ukijenga kilomita moja ya barabara, ni sawa na kujenga vituo vitatu vya afya, pamoja na kuweka vifaa tiba ndani yake. Kwa hiyo, niwaombe sana tutunze barabara zetu," anasema Dk. Samia.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS), Mohamed Besta anaeleza miradi hiyo iliyozinduliwa imekamilika Aprili mwaka huu, akiainisha imegahrimu shilingi bilioni 150.5 inayojumuisha ujenzi, ushauri na fidia kwa wenyeji, kazi iliyotekezwa na mkandarasi kampuni ya Kichina.

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa naye akatoa ufafanuzi kuwa, barabara ya Sumbawanga - Matai hadi Bandari Kasanga, inaunganishwa na nyingine inayokarabatiwa ya Matai - Tatanda - Kasesya yenye kilomita 50.

Hiyo inatarajiwa ikikamilika, itarahisisha usafiri na usafirishaji kutoka mpakani Kasesya Zambia, akisema Rais ameshatoa fedha za kuanza kazi hiyo.

**KWANINI KASSANGA?**

Bandari ya Kasanga iliyopo wilayani Kalambo mkoa wa Rukwa, ujenzi wake nao ulikamilika mwishoni mwa mwezi Aprili, 2020. Hiyo ni miongoni mwa bandari zinazomilikiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), katika Ziwa Tanganyika

Hiyo ni bandari ya kimkakati iliyoko kwenye mpaka wa Zambia na DRC na ya pili kwa ukubwa kwenye Ziwa Tanganyika, nyuma ya Bandari Kigoma.

Kimsingi, Bandari ya Kasanga ni mji mdogo ulioko wilayani Kalambo, Kusini-Magharibi wa Tanzania, mwambaoni mwa Ziwa Tanganyika, ikiwa na historia ndefu tangu utawala wa ukoloni wa Ujerumani, ikibatizwa jina la Bismarckburg.

Katika Sensa ya Watu na Makazi nchini mwaka juzi, wakazi wa mji mdogo Kasanga, walihesabiwa kuwa 13,281 na pana umbali wa kilomita 67 kutoka makao makuu ya wilaya ya Kalambo.

Hivi sasa, mji wa Kasanga umejengwa na Soko la Kimataifa la Samaki Kasanga na kuna mpango wa kufunga vyumba baridi vya kuhifadhi samaki, Kasanga na eneo la Muzi, kunufaisha vijiji jirani vitanufaika, huku kuiunganishwa na nchi jirani DRC, hata kufungua maradufu njia hiyo, ikitajwa hadi sasa malori mengi ya mizigo kwenda nchi hiyo jirani, kutoka bandarini Dar es Salaam.

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, anataja miradi mingine ya barabara iliyokamilika mkoani Rukwa ni ya Tunduma (Songwe) hadi Sumbawanga, kilomita 220 na Sumbwanga - Kanazi - Kizi - Kibaoni (km 151.6), zote ni za kiwango cha lami.

Mtendaji Mkuu wa TANROADS), Mhandisi Mohamed Besta, anasema ujenzi wa barabara hizo ni mwendelezo wa malengo ya serikali kujenga barabara kiwango cha lami, hadi sasa kilomita 802.55 zimekamilika, kati ya hitaji kilomita 1,286, sawa na asilimia 62.40.

Aidha, Bashungwa anaeleza mkakati wa serikali katika mwaka uliopo fedha 2024/25 mkoani Rukwa ni kuanza usanifu wa barabara ya Laela - Mwimbi - Kizombwe (Km. 93).

BIASHARA

# Mtaalamu muonja chai pekee EAC, elimu aliyopata darasani Uingereza mwaka mzima

- Anaweza kuonja vikombe 1,000 akagundua tofauti
- Asema chai bora huchumwa mkononi, mashine hazifai
- Mnywaji 'kuliko maelezo' akihisi kasoro arudi dukani

**Na Mwandishi Wetu**

Mzee Richard Mwakangale, ni miongoni mwa waonja chai (tea taster) wachache kuwapo nchini. Kwake kuonja chai iliyopikwa kwa takribani vikombe 1,000 ni jambo la kawaida.

Kwenye sekta ya chai amekuwamo kwa takribani miaka 30 akijipatia ujuzi London nchini Uingereza na aliporejea nchini, akawa tegemeo kati ya waonja chai wachache nchini.

Mzee Richard (74), sasa ni mstaafu, ingawa bado hayuko mbali na taaluma yake. Amebaki akiishi nayo, kudadisi unywaji chai na vigezo vyake, huku ikibaki kiburudisho kikubwa nyumbani kwake na kwa wageni wanaomtembelea.

Amekutana na Nipashe kwenye Maonyesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF), yaliyohitimishwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, Julai 13 mwaka huu.

Katika Banda la Bodi ya Chai Tanzania (TBT), kwenye maonyesho hayo, alifanya mazungumzo ya kina kuhusu zao la chai na mnyororo wake iliko shambani hadi mezani, ikidumu kuwa mlo na kiburudisho kikubwa duniani.

Kazi aliyoifanya kwa takribani miongo mitatu, inasadifu maisha yake, akiwa nyumbani kwake chai anayokunywa inapoletwa mezani, hubaini mara moja ubora wake, majani na daraja lake.

Asiporidhika nayo, huchukua hatua ya kuleta majani mapya dukani yakiwa yenye ladha aipendayo, vigezo ubora.

Mbali na maelezo yake, Bodi ya Chai nchini ina maelezo ya wazi na rasmi kuhusu zao hilo hususan kiafya, kwamba kisayansi mtu anayekunywa chai kabla ya kuungwa sukari, faida zake ni takribani tisa mojawapo ni kuimarisha afya ya akili.

Kwa Mzee Mwakangale, yafuatayo ndio mazungumzo yake na Nipashe, maswali na majibu, walipokuwa katika Viwanja vya Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara - Sabasaba, Dar es Salaam. Fuatilia:

**SWALIi:** Mara nyingi zao la chai halifahamiki kiundani, ila umaarufu wake upo mezani. Je, chai ni nini?



Richard Mwakangale (kushoto), akizungumza jambo katika Banda la Bodi ya Chai Tanzania (TB) kwenye Maonyesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF). **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

JIBU: Zao la chai lina mnyororo mrefu tangu shambani linapolimwa hadi kuwa chai inayonywewa. kwa ujumla, chai ni zao lenye thamani na kilimo chake huchagua mazingira.

Zao la chai kisayansi linaitwa 'camellia sinesensis'. Hili ndio jina la chai. Na mti wa chai unadumu sana. Ukishapanda unafanya 'prooning' ili mtu aweze kuchuma majani yake vizuri.

Zao la chai linaweza kudumu hata miaka 100 (karne moja). Nakumbuka kuna mashamba Kimbila, Tukuyu (Mbeya), ambayo tangu mimi nasoma shule ya msingi na mpaka leo bado yapo.

Shina la mti wa chai linaweza kuwa kubwa kama mguu, lakini linapofanyiwa 'pruning' (kupunguza majani) huku juu haliendelei kuwa kubwa. Ila kama halifanyiwi prooning, linaweza kuwa kubwa kama mti.

Zamani zao la chai lilipandwa kwa mbegu, lakini siku hizi wanapanda kwa kile kinachoitwa 'propagative vegetation' yaani unachukua tawi la chai unaliotesha, halafu linakuwa mti wa chai.

**SWALI:** Kwanini majani ya chai yanawekwa katika madaraja pale linapouzwa sokoni?

**JIBU:** Ubora wa chai unaanzia shambani. Inategemeana na 'spishi' (aina) au familia ya aina gani ya ule mti. Kuna chai ambazo zinaitwa 'chrono' ukiipanda chai inakuwa nzuri sana.

Sababu nyingine ya ubora wa chai, ni udongo tunaita 'Soil PH'. Udongo una maana sana katika ubora wa chai. Jambo lingine ni mvua, chai hustawi kwenye mvua, pia hutegemea na mwinuko (attitude). Chai ambayo imepandwa katika mwinuko mrefu, inakuwa na ladha nzuri sana na 'flavoured'.

Chai inapokuwa shambani inachumwa kwa mkono na huchumwa majani mawili na sindano au unachuma 'soft bunji', majani fulani malaini. Lakini siku hizi, wanachuma majani kwa kutumia vifaa maalum vya kuchumia. Hii inapoteza ubora wa chai, kwa sababu majani yanayochumwa na kifaa hicho mengi si yale yenye viwango au vitatu yaani, hesabu ya majani mawili na sindano. Ukichuma chai kwa mkono na kifaa, ubora ni tofauti.

Pia kwenye zao hili shambani, wakulima wamegawanywa kwa makundi mawili; wadogo na wakubwa. Mkulima mdogo shamba lake ni ekari tano hadi 10. Mfano sisi nyumbani kwetu kwa Mzee Mwakangale (John Mwakangale- Tukuyu), shamba letu ni la mkulima mdogo.

**SWALI:** Baada ya chai kuvunwa kutoka shambani, hatua gani hufuata?

**JIBU:** Chai ikivunwa inapimwa uzito ni kiasi gani ili atakapolipwa ijulikane ni malipo ya chai kiasi gani. Chai ikishavunwa shambani au ikichumwa inatakiwa ipelekwe haraka kiwandani.

Kwanini iende haraka kiwandani. Chai ina rangi ya kijani yaani lile jani lake kitaalamu ni 'green pigment'. Ile green pigment inatokana na 'chromophyll' ndio inafanya jani liwe la kijani. Ukiichukua jani na ukalivunja ndani, kuna 'enzyme' ambayo inakula ule ukijani na kubadili kuwa rangi ya kahawia.

Kwa hiyo mara tu jani linapochumwa tu likimbizwe kiwandani kabla halijaanza kubadilika kuwa kahawia. Inapocheleweshwa majani, yanaweza kutupwa kwa sababu ubora wa chai umepotea. Mara nyingi tu majani yatatupwa, kwa sababu hii.

Jani likiwa kiwandani linafanyiwa 'withering' kunakuwa na kitu mfano wa kitanda au kichanja, majani yanatandazwa yenye kilo 1,600 hadi 2,000. Hii ni hatua ya kukausha jani, kuondoa maji kwa sababu unaweza kupima jani kumbe uzito ule ni kutokana na maji.

**SWALI:** Je, kuna tofauti kati ya chai ya kijani (green tea) na chai nyeusi (black tea)?

JIBU: Tofauti ya chai nyeusi na kijani. inatokana na hatua za uandaaji kiwandani. Chai nyeusi ni baada ya kufanyiwa 'withering', lakini chai ya kijani ikitoka shambani wanaifanyia 'steaming' kuua enzyme na kuzifanya jani kubaki na ukijani wake.

Chai ya kijani ni maarufu zaidi kwa Wachina, wanatumia zaidi na wengine.

Hatua ya kunyausha jani lililotoka shambani katika kitanda au kichanja hicho, huchukua takribani saa 16 kwa kutumia upepo kama feni, ingawa ukaushaji wa asili wa jani la chai ndio hatua nzuri zaidi ikilinganishwa na hii inayotumiwa ya 'withering'. Lakini kufanikisha ukaushaji wa asili ni ngumu kwa sababu kunakuwa na kilo nyingi za majani.

Baada ya kukausha inafuaa hatua ya kukamua juisi kutoka jani, kitaalamu inaitwa 'rotorvane' kisha inapelekwa katika mashine ya CTC kirefu chake ni 'Crushing Tearing & Curling' kama vile wakinamama wanavyo 'curl' nywele zao.

Baada ya hapo inapelekwa 'fermenting' hii ni hatua muhimu na isipofanyika vizuri chai haiwezi kuwa nzuri.

Ukiweka muda mrefu tatizo na muda mfupi tatizo, lazima uzingatie muda maalum. Itafuata hatua ya 'dryer' kuikausha chai ikitoka hapo inakuwa nyeusi.

Baada ya hatua hizo inakuja hatua za madaraja inaitwa 'sorting' na madaraja hayo ni la kwanza ambalo ni BP1 (browser pekoe one); PF1 (pekoe fanning one); PD (pekoe dust); Dust One; Fanning na BMF (broken mixed fanning).

Madaraja haya ndio huamua soko na mahitaji yako. Zamani kulikuwa na masanduku. Unaifunga katika sanduku, lakini sasa hivi kuna 'bags' au tea bags na begi moja huchukua kilo 50 hadi 60 inategemeana. Mfano 'PD' huingia nyingi zaidi katika begi.

**SWALI:** Njia gani hutumika katika kuiuza chai ambayo pengine hufika hadi soko la nje?

**JIBU:** Kuna njia nyingi za kuuza chai, moja ni kwenye mnada wa kimataifa, upo Mombasa (Kenya) na hivi sasa nasikia Tanzania umeanzishwa mnada Kurasini.

Na mnada wa Mombasa ni mkubwa sana zinakuja chai dunia nzima na nimehudhuria sana kwenye mnada huo. Chai zinasafirishwa hadi katika ghala na mtu wa ghala anatoa sampo kwa madalali ambao nao wanaonja (tasting) wanaithaminisha chai na kisha wanapanga bei kulingana na kile alichokionja.

Kwa 'tea tasting' ndio maana yake hii na inauzwa kwa dola huko Mombasa. Baada ya kupanga bei wanaisajii chai mfano 'Katumba tea' ina daraja hili PF1 nauza shilingi 100 kwa kilo'...mnada utaendelea kwa ushindani kila mmoja anataja bei ya juu yake, mwingine shilingi 140 au 90. Muuzaji akiona bei mbaya anaiondoa (withdraw) mnadani, ili akauze pembeni asipate hasara.

Hatua nyingine ya kuiuza ni kuuza moja kwa moja, unaweza ukapeleka Ulaya, au kwa tea blenders, kama Chai Bora nao wanakwenda kui-brand (kuipatia kundi) na kuweka nembo zao.

Chai huwa inachukua unyevu haraka sana, ni lazima uifunike, yaani ina 'hygroscopic'. Mara nyingi, vifungashio vya chai huwa ndani vina aluminium ili maji yasiingie ndani.

Kama vile kahawa ukiiacha wazi utakuta inaganda. Chai isipotunzwa hivyo kwenye kifungashio ubora wake hupungua.

Ubora wa chai ni mnyororo kuanzia shambani.

**SWALI:** Unapozungumzia muonja chai 'tea taster' ina maana gani kwa lugha rahisi?

**JIBU:** Katika kuonja chai zipo hatua nne na lengo ni kuangalia ubora, ila ubora huanzia shambani. Kunakuwa na vikombe maalum vya kuonjea chai labda ni vya TBT au blenders, ni vya udongo na vyeupe.

Kuna kikombe, mfuniko kwa kila kikombe, kipimia majani (mizani maalum wa chai) na bakuli dogo.

Unachukua hicho kipimo, unaweka katika kikombe, majani, unachukua maji yaliyochemshwa, unaweka maji katika kikombe. Uingereza tulikuwa tunaonja chai hadi vikombe 1,000 chai ya dunia nzima!

Na hata nikionja vikombe 1,000 najua tofauti, kila chai daraja lake na ilikotokea ina alama yake nyuma labda, hii Tanzania, Rwanda. Baada ya dakika sita majani ya chai, maji katika kikombe utafunua. Maji utamwagia katika bakuli, makapi tutaweka kwenye mfuniko na chai nzuri hung'aa kama senti tano au kama kopa. Ukiweka juu tu kwenye bakuli lazima ing'ae.

Halafu unaangalia jani lenyewe limetengenezwaje? Kwa macho utajua hii nyeusi, kahawia tuna teminoloji zetu kama za kidaktari.

Mimi muonjaji ndio natoa maoni na kuipa thamani chai. Unarudi katika ule mchuzi wa chai, ukiangalia sana ni kama manjano hivi vitu ambavyo vinaleta ladha. Kama vile mchele wa Kyela, utakuta mchuzi wa chai mzito au mwepesi na rangi yake je?

Tutaweka na maziwa kidogo, ili unye rangi kwa sababu wapo watumiaji wanaotumia maziwa na majani. Utajua hii ni nzuri.

Baada ya hapo unaweka bei. Unakuta katika uonjaji upo pekee yako au mko wengi. Matokeo ya uonjaji ndio unaona daraja la chai na ubora wake kwa sababu kuna chai, ambayo ukiionja unajua kabisa hii ilipitia hatua ya kuungua. Kumbuka kila unapoonja unatema, unatema eneo maalum, kisha huonjwa nyingine hata 1,000.

Mfano chai inayolimwa India milima ya Himalaya ndio bora zaidi, inaitwa 'darjeeng' ni ghali duniani ni nzito ukiweka katika kikombe inanukia kama vile ina moshi. Kuna chai inaitwa 'Assam tea', na kuna nyingine pia inalimwa Kusini mwa India ukiweka kwenye kikombe nyepesi ila bora.

Ukienda Sri Lanka chai yake ukiweka katika kikombe inang'aa kama dhahabu, ina njano nyingi. Nimeonja zote hizo hii inatemea na ilivyolimwa kwenye milima hali ya hewa.

Kwingine kwenye chai nzuri

Inaendelea Uk 14

## TAFAKURI YA MLALAHOI

### Sare za bodaboda na ufumbuzi wa ajali!




HIVI karibuni nilisikia habari njema kabisa zikihusu 'maofisa usafirishaji' wa Jiji la Dar es Salaam, kuzinduliwa sare zao za kazi.

Ukisikia maofisa usafirishaji utadhani pengine ni wa Kampuni ya Mabasi yaendayo Haraka (UDART).

Pengine utadhani ni maofisa wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) au pengine wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) hasa wa treni iliyojizolea umaarufu haraka ya SGR au labda wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji, la hasha, ni madereva wa bodaboda.

Waheshimiwa hawa, ni wale wasiojua kuwapo sheria za usalama barabarani, kwamba wao wanafanya shughuli zao chini ya Mhimili moja kwa moja na wasisumbuliwe na polisi au ndugu wa polisi tunaowaita polisi jamii.

Maofisa hawa, hata wanapokosea barabarani, faini yao haifanani wala kulingana na ya dereva wa chombo kingine cha moto kinachopita ardhini, wao ni waheshimiwa, lazima waheshimiwe na ndiyo sababu juzi kati wakazinduliwa sare zao.

Nia yao ni kwamba wajulikane na waheshimiwe, hata wakivuka kivuko cha pundamilia bila kusubiri waenda kwa miguu wakatize, hata wasipoangalia taa nyekundu zikiwazuia kupita wao haiwahusu, kinachowahusu ni sare, kwamba ukiwaona tu hata wakivunja sheria achana nao wana sare hao.

Ukiona kwamba sasa ni lazima walipe faini kwa kuwa wamevunja mtu mgongo kwa makosa au miguu au hata kuua, basi faini isifike Sh 30,000 kama ya dereva wa gari anapokuwa amefanya yake barabarani ambayo ni pamoja na kuzidisha mwendo akafikia kilometa 51 kwa saa badala ya 50.

Ili mradi ana sare yake, hata kama hakuvaa kofia ngumu, ofisa usafirishaji mwache kabisa afanye kazi yake, hata ukijipendekeza ukamwona anapiga muziki mnene kwenye boda yake haikuhusu, kwani ni kama aliyefunga honi ya lori na vimulimuli chekwa, haikuhusu huyu ni mheshimiwa.



**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008 barua pepe:kulangwasos@gmail.com

Mtanzania kama mimi unakaa unajiuliza, baada ya kuona yote hayo kwa dereva wa bodaboda mheshimiwa sana ofisa usafirishaji, kwa nini hachukuliwi hatua na kumdhibiti ili uhuni anaofanya barabarani ukome?

Ili mradi mtu kakosa la kufanya akanunua pikipiki yake, akaweza kuipiga teke ikawaka, akanyoosha usukani kama baiskeli na kupakia mshikaki, basi huyo tayari ameingia kwenye kundi la waheshimiwa maofisa usafirishaji na kukaa juu ya sheria pale.

Tunashuhudia na kuambiwa jinsi hospitalini MOI walivyojaa waheshimiwahawa bila miguu na wengine mikono na hata macho, kutokana na uzembe waufanyao barabarani na kusababisha ulemavu wa kudumu kama si vifo kwa abiria wao.

Tunashuhudia jinsi barabarani kulivyochafuka na utitiri wa mapikipiki yatoayo moshi mchafu na makelele ya honi za mabasi na malori zilizofungwa kwenye bodaboda hizo, tunaona jinsi pikipiki zilivyobadilishwa na sasa kuitwa 'SchoolBodas' na kukaribia kufunika 'School-Buses'. Naambiwa hapa, pikipiki zikigawanywa kila Mtanzania anapata moja!

Wazazi tunaangalia, polisi wanaangalia, viongozi wanaangalia, wenye shule zao wanaangalia, kwa sababu waheshimiwa maofisa usafirishaji wako kazini na tena wakati huu tukielekea uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu, wanabadilika na kuitwa waheshimiwa wapiga kura wetu. Waguse uone cha moto!

Hivi Watanzania mnajua kuwa ipo sheria inayokataza watoto wa umri wa chini ya miaka tisa kupanda pikipiki? Mnajua au hamjui? Bila shaka hamjui na kwa kuwa hamjasikia bodaboda kakamatwa kwa kubeba mtoto wa miaka tisa na kushuka, basi mnaona ni mwujiza tu.

Ni hivi, kuna sheria inakataza katukatu mtoto wa miaka tisa kurudi chini kupanda bodaboda au pikipiki iwayo yote ile, isipokuwa bajaji. Kwanza, mtoto hawezi kujishikiza kwenye pikipiki; pili, miguu yake ni mifupi hawezi kufikia pedeli za pikipiki na kukanyaga, na tatu, nani alishaona kofia ngumu za watoto? Sijui kwa mbilikimo inasemaje sheria!

Lakini pia unakuta dereva wa boda kampakia mtoto mbele kwenye tangi la mafuta, bila kizuizi chochote huku yeye kajivalia jaketi zito la kuzuia upepo, kofia ngumu kama ni lazima lakini pia miwani ya kuzuia vumbi na upepo, mtoto je? Hicho kifua chake kinahimili hayo? Macho je? Pua?

Polisi wetu wa usalama barabarani wanayajua haya kabisa, lakini wanayatekeleza kinadharia, na ndiyo sababu hujasikia kesi mahakamani ya kubeba watoto kwenye boda na ndiyo kwanza mishikaki yao ni mingi kwani wanakaa wengi kwenye boda moja. Mpo Wabongo?

BIASHARA

# Kilio bei ya ufuta, ghafla kilivyogeuka tabasamu kwa wakulima Mkuranga

**Na Yasmine Protace,**
MKURANGA

KATIKA kuhakikisha wakulima wananufaika na mazao yao kupitia minada, serikali imekuwa ikiboresha mazingira ya minada yake, ili wakulima waweze kunufaika nayo.

Awali, wakulima hao walilalamika hawanufaiki nayo kutokana na kuuzwa kiholela kutokana na kutokuwa na usimamizi sahihi.

Hivyo, serikali imeweka taratibu za minada ,ikiwamo na kuwapatia wakulima ruzuku za pembejeo kwa ajili ya kuzalisha kilimo na chenye tija.

Serikali ilianzisha mnada kwa njia ya mfumo unaoitwa TMX, ambayo wakulima waliulalamikia mfumo huo kwao wanunuzi na kusababisha mazao kuuzwa kwa bei ndogo au kutonunuliwa.

Hata hivyo, baada ya kuulalamikia mfumo huo, serikali ikachukua hatua za haraka kuboresha, sasa wakulima hao katika baadhii ya maeneo walikiri ahueni ya bei inayoongezeka, kwa wanunuzi wanaofika maghalani.

Hiyo ikashudiwa katika Msimu wa Tano wa Mnada wa Ufuta, ambako Nipashe ilikuwapo katika mnada wa Kingoma wilaya Mkuranga, mkoani Pwani, ufuta ukiuzwa wote uliokusanywa ghalani.

Meneja wa Chama cha Ushirika Mkoani Pwani (CORRECU), Hamis Mantawela, anasema huo ni mnada wa tano wa ufuta kufanyika hapo, ambako zaidi ya tani 1,000 za mazao zilikusanywa na kuuzwa.



Gari likishusha ufuta katika ghala kwa ajili kuuzwa mnadani katika mkoa wa Pwani. **PICHA: YASMINE PROTACE.**

"Tani 1,195,189 zimekusaywa Mkuranga na kuuzwa kwa kilo moja shilingi 3500.3" anasema Mantawela.

Anaongeza kuwa ni wajibu wa wakulima wa ufuta kuleta ufuta katika minada miwili iliyosalia ili waweze kuuza.

Matawela anasema, kwa sasa bei ya ufuta imepanda tofauti na minada ya nyuma, kilo moja iliuzwa shilingi 301,17 huku mnada wa nne ufuta uliuzwa shilingi 3,280.13.

Anasema serikali imetoa mafunzo ya siku tatu ili viongozi wa vyama vya amccos kujua jinsi ya kuitumia mifumo hiyo.

"Mafunzo yaliandaliwa ya siku tano,lakini yamefanyika ya siku tatu,hayo yaliyobakia ya siku mbili yataendelea," anasema.

Anaongeza kuwa, mafunzo hayo yatasaidia hata katika mnada wa mbaazi ambao utafanyika hivi karibuni.

Meneja huyo anasema, mnada usaswa umebaki utakaofanyika mara mbili, hivyo anawaonya watakaouza ufuta kwa njia za panya watachukuliwa hatua, akionya "viongozi wa vyama vya ushirika wasifurahie ufuta kutoroshwa."

"Wapo watu waliogoma kuleta ufuta katika mnada wanategemea mnada uishe ili wautoreshe ,tutakaa katika vizuia ili kuwakamata wale wanaotaka kuutorosha ufuta," anasema.

Anaongeza kuwa, atakayekamatwa anatorosha ufuta, atalipishwa faini ikiwamo kuchukuliwa gari na ufuta aliobeba.

Kwa mujibu wa Mantawela. baada ya mnada wa ufuta, unaofuata ni mnada wa mbaazi na kisha utafuata mnada wa korosho.

Anasema wataanza kutembelea mashamba ya mbaazi, ili kujua idadi ya mbaazi zilizopo katika mashamba.

"Maghala yataendelea kuwapo, ila kama mbaazi hazipo ni jukumu la viongozi kusema,"anaeleza, huku akiwa na ushauri kwa wakulima kuleta ufuta mnadani na endapo watausubiri mnada wa mwisho, hatari yake bei inaweza kuwa mbaya na wakashindwa kunufaika na mauzo kama ilivyo sasa.

"Wakulima wajue mnada wa mwisho huwa una mambo mengi sana, unaweza ufuta usifike idadi ile ambayo unajua ndio mlioikusanya maana kunakupasuka mifuko ufuta ukamwagika chini na kufanya kilo kupungua, hivyo nawashauri wakulima msifiche ufuta majumbani mkauleta mnada wa mwisho," anasema.

Mwenyekiti wa CORECU mkoa wa Pwani, Mussa Mng'eresa, anawaasa wakulima kuwa bei ya ufuta imepanda na vyema wapelekwe mavuno yao katika vyama hivyo, kufanyike biashara ya mavuno yao.

Anasema, awali biashara ya ufuta ilishuka sana na ghafla kutoka kilo shilingi 4000 hadi shilingi 3000.

Omary Mussa, Mwenyekiti wa AMCCOS Kibaoni, anasema bei ya ufuta imepanda na kuna tabia ikiwa chini, wakulima huwa hawajitokezi katika maghala kuleta ufuta wao.

# Mtaalamu muonja chai pekee EAC, elimu aliyopata darasani Uingereza mwaka mzima

Inatoka Uk 12

Rwanda inalimwa kwenye milima, chai Burundi nayo sawa, Kenya, Malawi pia nzuri na Tanzania tunajitahidi. Utengenezaji, aina ya mmea, udongo, hali ya hewa, kulima kwenye miinuko, vinachangia ubora wa chai.

Nilikuwa Uingereza nikiona na kujifunza chai aina mbalimbali katika mnada. Kilimo cha chai lazima kiwe jirani na kiwanda, kulinda ubora. Ndio maana magari ya kiwanda huzifuata chai shambani.

**SWALI:** Kwanini chai ni muhimu kwa binadamu?

**JIBU:** Chai ni muhimu na katika soko chai inawekwa kulingana na mahitaji ya watu. Tunakunywa chai kwa sababu ya 'caffein' ila ni ndogo ikilinganishwa na iliyomo kwenye kahawa.

Wataalamu wanasema 'caffein' inasaidia katika mfumo wa fahamu, labda kichwa kinauma, ukinywa inasaidia.

Pia, katika mfumo wa hewa au umechoka, inasaidia hata katika mfumo wa moyo.

**SWALI:** Je, uonjaji chai ni fani inayosomewa darasani au unatumia uzoefu?

**JIBU:** Kuonja chai 'tea tasting' nilikwenda Uingereza mwaka 1975 na masomo haya yalifadhiliwa na British Council. Serikali ya Uingereza ilinipeleka kusoma kwa mwaka mmoja. Nilikuwa nakaa na madalali wa chai London huko wakanifundisha namna ya kuonja chai.

Baadae, nikaenda Brooke Bond ni kampuni kubwa na wataalamu wakubwa wa chai duniani. Kampuni tangu miaka ya 1800.

Baada ya hapo nikarudi Tanzania, Watanzania waliopata nafasi ya kwenda huko ni wanne tu, nikiwamo mimi. Wengine wameshafariki.

Awali mwaka 1972 niliajiriwa Mamlaka ya Chai nikiwa Manager Trainee katika kiwanda cha Majani ya Chai Lupembe, Njombe na baada ya hapo ndio nikaenda kujifunza 'tea tasting', ni taaluma ndogo katika mambo ya chai. Mwaka 1975 nilikwenda kusomea Tea Tasting and Marketing (uonjaji chaio na masoko yake).

**KILIMO CHA CHAI**

Zao la chai ni miongoni mwa mazao ya kimkakati nchini, likianzia mwaka 1902 kutoka kwa Mjerumani, kwa mujibu wa Bodi ya Chai Tanzania.

Mwaka 1903, likaanzia kupandwa Nyanda za Juu Kusini kama vile Tukuyu wilayani Rungwe, Njombe, Ludewa, Kilolo na Mufindi. Kadhalika Tarime, Korogwe, Kushoto, Bukoba, Kilimanjaro na Muheza.

Nchini kuna viwanda 24 vya usindikaji, kati ya hivyo vikubwa ni 22 na vilivyosalia vidogo. Umiliki wa ubia ni katika viwanda vinne. Viwanda hivyo vinaweza kusindika tani 69,455 za chai kavu kila mwaka.

Uzalishaji chai kutoka kwa wakulima kwa sasa nao ni tani 37,000 kwa mwaka huku, asilimia 38 kati ya mahitaji hayo yalizalishwa na wakulima wadogo.

Asilimia 85 ya chai zilisindikwa nchini na kuuzwa moja kwa moja kupitia soko la Mombasa, Kenya kazi inayofanywa na madalali. Asilimia 15 iliyosalia ni kwa matumizi ya ndani.

TBT inafafanua kwamba, chai ni kinywaji cha pili kinachonywewa kwa wingi baada ya maji. Ina virutubisho na madini ya manganese, zinki, potassium, vitamini B na E, pia kemikali iitwayo 'polyphenol' inayozuia uwezekano wa kupata saratani na kiharusi.

Pia, chao inaimarisha meno, mmeng'enyo wa chakula, huongeza umakini inapambana saratani ya matiti, ngozi, tumbo na ngozi, huku utafiti ukionyesha inakata kiu na vikombe sita hadi nane kwa siku, huongeza maji mwilini sawa na idadi hiyo ya vikombe.

Mwakangale anasema, katika Afrika Mashariki walikuwa hawazidi watano, kwa sasa yuko peke yake, ameshriki sana minada mbalimbali ya chai, ikiwamo Mombasa, Kenya.



## HABARI DODOMA

# Ikungi wanahitaji bil.11/- ukarabati miundombinu

**Na Thobias Mwanakatwe,**
IKUNGI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Ikungi mkoani Singida inahitaji zaidi ya Sh. bilioni 11 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya sekta ya elimu, afya na ofisi za serikali za vijiji na kata.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Justice Kijazi alieleza hayo juzi katika ziara yake ya kusikiliza kero za wananchi na watumishi kwenye kata za Misughaa, Kikio na Ntuntu.

Alisema katika halmashauri hiyo kuna baadhi ya shule chakavu zinazohitaji kukarabatiwa, ujenzi wa madarasa, ofisi za serikali za kata na vijiji na zahanati ambapo ili kukamilisha ujenzi huo kunahitajika kiasi hicho cha fedha.

Kijazi alisema katika kuhakikisha fedha hizo zinapatikana katika mwaka wa fedha wa mwaka huu, halmashauri imeanza kutenga fedha kidogo kidogo katika mapato yake ya ndani wakati nyingine zinapatikana kutoka serikari kuu, wafadhili na wadau mbalimbali wa maendeleo.

Alisema katika Kata ya Misughaa halmashauri imetenga Sh. milioni 80 kwa ajili ya kutatua kero mbalimbali ambapo kati ya hizo Sh. milioni 20 zitatumika kumalizia ujenzi wa bweni la wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Dk.Sheni.

Katika shule hiyo, Waziri wa Habari na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alitoa mchango wa saruji mifuko 400 kukamilisha ujenzi wa bweni la shule hiyo.

Aidha, Kijazi aliagiza ujenzi wa vyoo vya Zahanati ya Misughaa ukamilike haraka ili kupunguza adha iliyopo na kukarabati baadhi ya vyumba vya madarasa pamoja na kuhakikisha madawati yanatosheleza kwa wanafunzi.

Hivyo, alipongeza juhudi za Shule ya Sekondari Dk. Shein kutekeleza maagizo ya serikali ya wanafunzi kupata chakula wakiwa shuleni kwani wananchi wametekeleza kwa kiwango kikubwa na wana akiba ya chakula cha kutosheleza mpaka mwaka 2025.

Naye, Ofisa Utumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Jonas Lutiga aliwataka watumishi kufuata maadili ya kiutumishi kuanzia nidhamu ya mavazi na utekelezaji wa majukumu yao ya serikali ili kukuza maendeleo katika halmashauri hiyo.



Maofisa wa idara mbalimbali za Halmashauri ya wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma, wakizungumza na mkazi wa kijiji cha Majereko, Melea Obed ambaye ni mlemavu wa viungo aliyenufaika na msaada kutoka shirika lisilo la kiserikali la Brac Maendeleo Tanzania, uliomwezesha kuwa mjasiriamali na kuachana na kazi ya kuombaomba mitaani, walipomtembelea nyumbani kwake juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# AG aitaka CMA kutoa elimu migogoro ya kikazi

**Na Halfani Chusi**

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali (AG), Jaji Dk. Eliezer Feleshi ameitaka Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), kutoa mafunzo kwa waajiri na waajiriwa ili kupunguza migogoro ya kikazi inayotokana na ukosefu wa elimu.

Alitoa wito huo mwisho mwa wiki alipotembelea banda la CMA katika banda jumuishi la Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake katika Maonesho ya 48 ya Sabasaba yaliyotamatika siku chache zilizopita jijini Dar es salaam.

Aidha, aliitaka tume kuwa na mifumo inayosomana na mahakama ili kuweza kusaidia katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali zinazofanywa na mahakama kwa kushirikiana na tume.

Naye, Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma alisema atatetea CMA ili ipate bajeti ya kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kusogeza huduma zake karibu na wananchi, huku akiipongeza kwa kufanya kazi nzuri katika utatuzi wa migogoro kwa watumishi wa umma.

Mkurugenzi wa CMA, Usekelege Mpulla, alisema tume inatarajia kuanza matumizi ya mfumo wa kusajili mashauri kwa njia ya mtandao unaofahamika kama 'Online Case Management System' ambao utamuwezesha kila mwananchi kusajili mgogoro wake popote alipo.

Alisema CMA imejipanga kuhakikisha huduma za tume zinapatikana katika ngazi ya wilaya na tayari inatarajia kuanzisha tume inayotembea itakayowezesha wananchi kupata huduma na haki kwa wakati.

# 'Chamwino changamkieni kilimo cha mbaazi'

**Na Peter Mkwavila,**
CHAMWINO

WAKULIMA wa Kijiji cha Mlowa Barabarani Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma wametakiwa kuchangamkia fursa ya kilimo cha mbaazi kwa ustawi wa afya zao na kujiongezea kipato.

Mkurugenzi wa Shirika la Wakulima, Wazalishaji Mbegu Dodoma (DASPA), Aithan Chaula alitoa wito huo juzi wakati wa mafunzo kwa wakulima kuhusu kilimo bora cha mbaazi yaliyofanyika wilayani hapa.

Chaula alisema mafunzo hayo yalitolewa na DASPA kwa kushirikiana na Kituo cha Kimataifa cha Uboreshaji wa Mahindi na Ngano (CIMMYT) na Halmashauri ya Chamwino.

Alisema kuwa mbaazi ni zao linalofanya vizuri baada ya mvua kuisha.

Alisema kuwa mbaazi ni zao jamii ya mikunde, ni chanzo cha viini lishe vya protini kwa binadamu na wanyama, linavumilia ukame pia ni chanzo cha mapato na kurutubisha udongo.

Aidha, alisema mbaazi zimekuwa zikitumika kama mboga pia kutengeneza bagia, biskuti, keki, sambusa, uji na vyakula vingine.

Alisema bei ya kilo moja ya mbaazi ni Sh. 3,000, hivyo ni vyema wakulima wakachangamkia fursa hiyo.

Naye Ofisa Kilimo Kata ya Mlowa Barabarani, Winnie Ndahani aliwataka wakulima wa mbaazi kuchamkia kilimo hicho ili kuongeza uchumi ngazi ya familia pia uimarisha afya.

Mtaalam wa mbegu kutoka Halmashauri ya Wilaya Chamwino, Iveta Paul alisema ni vyema wakulima wakatumia mbegu bora kwa uhakika wa kipato.

# Naibu Katibu Mkuu ataja siri kudhibiti utoroshaji madini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Madini, Msafiri Mbibo amesema ujenzi wa mifumo bora katika uchimbaji na biashara ya madini, maboresho ya sheria, sera na usimamizi endelevu, ni chachu ya udhibiti wa vitendo vya utoroshaji madini nchini.

Aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika mahojiano maalum.

Mahojiano hayo yalitokana na taarifa za utafiti mpya zilizotolewa na Shirika la Swiss Aid kuitaja Tanzania kama nchi iliyofanikiwa kudhibiti vitendo vya utoroshaji madini hususani dhahabu ikilinganishwa na nchi nyingine.

Kwa mujibu wa utafiti huo, zaidi ya tani moja hutoroshwa kila siku kutoka mataifa yenye utajiri mkubwa wa madini dhahabu Afrika, huku zaidi ya nusu ya dhahabu inayouzwa kimagendo inatokana na shughuli za uchimbaji mdogo. Aidha, utafiti huo ulionesha kwamba mwaka 2022 pekee dhahabu tani 435 zenye thamani ya zaidi ya Dola za Marekani bilioni 30 zilitoroshwa kupelekewa katika mataifa ya Uswis na India.

Mbibo alisema kuwa sababu nyingine iliyosababisha Tanzania kuwa kinara katika eneo hilo ni kutokana na uwepo wa masoko ya madini na vituo vidogo vya ununuzi wa madini ambayo yamesaidia kurahisisha biashara ya madini, kuwepo kwa uwazi katika masoko hayo, uhakika wa masoko kwa wachimbaji pamoja na uwepo wa bei elekezi.

"Hivi sasa tuna jumla ya masoko 42 na vituo vidogo 100 vya ununuzi wa madini nchi nzima, suala ambalo limerahihisha kwa kiasi kikubwa biashara ya madini kwa wachimbaji wadogo. Serikali ilifikia uamuzi huu baada ya kufanya utafiti na kubainika kwamba ukosefu wa sehemu za kuuzia madini kwa wachimbaji wadogo unasababisha uwepo wa vitendo vya utoroshaji madini," alisema Mbibo.

Alitaja sababu nyingine ni mazingira wezeshi kwenye biashara ya madini katika kila hatua hadi kumfikia mlaji wa mwisho, uwepo wa kikosi maalum cha udhibiti wa vitendo vya utoroshaji madini kinachofanya kazi nchi nzima pamoja na ukaguzi wa mara kwa mara. Alisema sababu nyingine ni kutokana na kurasimishwa kwa shughuli za uchimbaji mdogo, utoaji wa elimu endelevu na uhamasishaji wa umma na wadau.

Nyingine ni serikali kuwa mbia na mwezeshaji wa wachimbaji wadogo kupitia huduma za uchorongaji zinazotolewa na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na huduma za uchenjuaji kupitia vituo vya mfano.

Vilevile, alisema utaratibu uliowekwa wa Wizara ya Madini kukutanana, kuzungumza na wadau kupitia makundi mbalimbali imesaidia kubaini changamoto na kutafuta suluhu.

Akizungumzia mikakati ya kuendeleza sekta alisema mpango wa serikali kurejesha minada ya madini ya vito na maonesho ya madini ya vito ambayo yatatoa nafasi ya wanunuzi na wauzaji kufanya biashara.





# Majengo shule iliyojengwa 1973 hatarini kuanguka

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAISHA ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Izumbwe Two iliyopo Kata ya Iwiji Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya yako hatarini kutokana na uchakavu na nyufa kwenye madarasa wanayosomea.

Kwa mujibu wa Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Wilson Ipyana ina wanafunzi 460, madarasa sita na kusababisha msongamano wakati wa masomo.

Hayo yalibainika juzi wakati wa ziara ya Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza ya kukagua miradi ya maendeleo, kusikiliza kero za wakazi wa jimbo hilo na kushuhudia moja ya majengo hayo limeegeshwa miti.

Mwalimu Ipyana, alisema shule hiyo iliyojengwa mwaka 1973, serikali haijawahi kuifanyia ukarabati zaidi ya wananchi ikiwemo kufukia mashimo.

Alisema madarasa yote hayana milango wala madirisha, hivyo afya za wanafunzi kuwa hatarini katika kipindi cha baridi kali.

"Kwa sasa wananchi wanaendelea kufyatua matofali kwa ajili ya kuongeza jengo moja la vyumba vya madarasa ili angalau tupunguze tatizo hili, mpaka sasa wamefyatua matofali 25,000 na wanaendelea," alisema Ipyana na kuongeza:

"Haya majengo yaliyopo ni ya muda mrefu sana na ndio maana yamechakaa kiasi hiki, hata ofisi ya walimu haifanani kabisa na kazi wanayoifanya."

Mwenyekiti wa Kijiji cha Izumbwe Two, Tex Kibona, alisema pamoja na uchakavu wa majengo ya shule hiyo, inakabiliwa na uhaba wa madawati, hivyo kuwalazimu wanafunzi kusongamana kwa yale machache yaliyopo huku wengine wakikaa chini.

Kibona, alisema yanahitajika zaidi ya madawati 60 ambayo hata yakipatikana kwa sasa itakuwa vigumu kuyaweka kwenye madarasa kutokana na ufinyu wa nafasi.

Alisema madarasa wanayokusudia kuyajenga ndimo watakamoweka madawati, hivyo kupunguza msongamano wa wanafunzi uliopo.

Mbunge Njeza, alisema shule hiyo ni miongoni mwa ambazo ziko kwenye Mpango wa Kuboresha Elimu ya Awali na Msingi (BOOST) ambao ni sehemu ya miradi ya lipa kulingana na matokeo.

Alisema fedha za mradi huo zimechelewa kufika katika shule hiyo na ni sababu ya mradi huo kuchelewa kujengewa madarasa na nyumba za walimu.

"Tumepita pale shuleni kwa kweli hali yake ni mbaya sana, nimeona kuna ukuta mmoja pale unataka hata kudondoka, nimuombe mkurugenzi tufanye utaratibu ili turekebishe pale tusije tukapata ajali ya watoto wetu," alisema Njeza.

Kuhusu uhaba wa madawati, alimuomba mwenyekiti wa kijiji hicho kutafuta miti na mashine ya kupasulia mbao na kuahidi kuchangia mafuta na kutumia mafundi wa mitaani kutengeneza samani hizo.



Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Maryprisca Mahundi (katikati mwenye gauni la batiki), akifurahia jambo na wanafunzi pamoja na wafanyakazi wa Chuo Kikuu cha Katoliki Mbeya (CUoM), aliposhiriki kongamano la mwaka mmoja wa Chuo hicho, hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wasakwa kwa kuuza ushoroba

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI ya Mkoa wa Mbeya imeliagiza Jeshi la Polisi kuwasaka na kuwakamata zaidi ya wakazi 10 wa Kata ya Kambikatoto wilayani hapa kwa tuhuma za kuuza eneo la mapito ya wanyama (Ushoroba).

Agizo hilo lilitolewa mapema wiki hii na Mkuu wa Mkoa huo, Juma Homera baada ya kubaini kuwa wakazi hao wanadaiwa kuuza eneo hilo kwa wafugaji jamii ya Wasukuma.

Homera, alisema kuuzwa kwa eneo hilo linalounganisha Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Pori la Akiba la Rukwati/Piti na Hifadhi ya Taifa ya Katavi kusababisha vurugu kati ya binadamu na wanyamapori.

Alisema wakazi hao wakiongozwa mtu mmoja (jina tunalo), wanadaiwa kumuuzia mfugaji eneo hilo kwa Shilingi milioni 10 na kuanza kujenga boma kwa ajili ya kufugia.

Alisema eneo hilo limehifadhiwa kwa muda mrefu na serikali lakini wakazi hao waliamua kuliuza kinyemela kwa maslahi yao binafsi na kuzua vurugu kwa maisha ya wanyama.

"Sasa naagiza watu hawa wote wakamatwe na waswekwe ndani na uzuri ni kwamba Mkuu wa Wilaya yupo hapa na amelichukua hili, naamini atasimamia na kuhakikisha wanashughulikiwa kwa mujibu wa sheria," alisema mkuu huyo wa mkoa.

Alisema endapo viongozi hao hawatachukua hatua dhidi ya wahalifu hao, atawashughulikia wao kwa mujibu wa sheria za utumishi wa umma.

Aliwataka wakazi wa maeneo ya jirani na hifadhi kuheshimu mipaka ili kuhakikisha hifadhi zinaendelea kustawi na kunufaika kwa kuwauzia watalii bidhaa wanazozalisha.

# CCM, wawekezaji kushirikiana

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimeahidi kuendelea kushirikiana na wawekezaji nchini kuwaletea wananchi maendeleo.

Ahadi hiyo ilitolewa juzi na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu CCM na Mlezi wa Mkoa wa Njombe, Halima Mohamed Mamuya wakati akiweka jiwe la msingi ujenzi wa soko la wakulima wilayani hapa utakaogharimu zaidi ya Shilingi milioni 400.

Mamuya, alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameleta wawekezaji nchini kushirikiana na serikali kuwaletea wananchi maendeleo.

"Hakuna jambo ambalo linaweza kufanywa na mtu mmoja peke yake kuleta maendeleo ya kweli, tunapaswa kushirikiana wananchi na wawekezaji wa nje ya nchi na kusonga mbele kwa pamoja," alisema.

Aliwashukuru wakazi wa Wilaya ya Njombe kwa kutekeleza sera ya uwekezaji ya kujenga uchumi bora wa Tanzania.

"Kila mahali mnapoona panaweza kuleta uwekezaji utakaosaidia jamii, utakaosaidia wawekezaji wenyewe na utakaojenga uchumi wa chama chetu cha Mapinduzi, msisite kufanya hivyo," alisema Mamuya.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Njombe, Deo Sanga aliwapongeza wawekezaji kwa kushirikiana na chama hicho kujenga maduka hayo.

Mbunge wa Njombe Mjini, Deo Mwanyika, alisema wafanyabiashara wa Njombe ni sehemu ya uwekezaji wa soko hilo. "Suala hili ndilo linatofautisha watu wa Njombe na mikoa mingine kwa sababu ni watu wa kujitoa sana na ni ambao wanataka na kupenda maendeleo sasa soko hili tunasema limewekwa na wawekezaji kutoka Njombe na sio mbali," alisema Mwanyika.

Mtunza hazina wa soko kuu, Mwinga Ngataulila, alisema vikao vya kamati ya siasa vya mwaka 2022/23 viliazimia lijengwe soko la wakulima kwa ajili ya wajasiriamali wadogo wadogo wa chama hicho wa Njombe.

Mwenyekiti wa soko la wakulima mjini Njombe, Rehema Hongoli, alisema waliamua kujenga soko hilo baada ya miundombinu iliyokuwepo awali kuchakaa na kuzingirwa na mafuriko wakati wa mvua.



# Wadau uvuvi, utalii watakiwa kuhifadhi matumbawe

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR.

MKURUGENZI wa Idara ya Uhifadhi wa Bahari Zanzibar kutoka Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, Dk. Makame Omar Makame amewataka wadau wa uvuvi na utalii kuyahifadhi maeneo ya matumbawe ya bahari, ili kukabiliana na mabadiliko tabia nchi.

Alitoa wito huo juzi wakati akizungumza na wadau wa uvuvi wa Unguja na Pemba katika mafunzo ya siku moja yanayohusu uhifadhi wa matumbawe kupitia mradi wa hifadhi matumbawe.

Alisema matumbawe ni rasilimali muhimu katika sekta ya uvuvi nchini kutokana na idadi kubwa ya watalii wanaofika nchini wanatembelea maeneo hayo kwa ajili ya kufanya shughuli mbalimbali za kitalii.

Alisema kuwa mbali na matumbawe kutumika kwa shughuli za kitalii pia yanatumika kwa ajili ya uvuvi kutokana na maeneo hayo kuzalisha samaki wengi na wavuvi kuweza kunufaika, hivyo ni vyema kuyahifadhi ili yaweze kuwaletea tija.

Alisema kuwa kutokana na umuhimu wa matumbawe idara kupitia Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi imeyahifadhi maeneo 14 kwa Unguja na Pemba yenye matumbawe mengi.

Alisema saba kati yao tayari yameshawekwa alama kwa ajili ya kuyahifadhi ili kutumika kwa shughuli mbalimbali ikiwemo ya kitalii ili kuingiza pato la taifa.

Dk. Makame akitaja sababu ya kuyahifadhi maeneo hayo 14 ni pamoja na kuwa na matumbawe mazuri hivyo wameona wayahifadhi ili yasiendelee kuharibiwa.

Mratibu wa mradi wa hifadhi matumbawe nchini, Godfrey Ngupula alisema lengo la mradi huo ni kukuza uwelewa wa hifadhi wa matumbawe kwa wadau mbalimbali. Alisema wameona kuna uharibifu mkubwa ukifanyika katika maeneo ya hifadhi ya matumbawe, hivyo wamelazimika kutoa elimu kwa wadau mbalimbali ili kuyatunza na kuyatumia kwa ajili ya kupata tija.

Akizungumza athari ya kutohifadhiwa kwa matumbawe, alisema kwa Tanzania zaidi ya asilimia 80 ya wavuvi wanategemea matumbawe kwa ajili ya uvuvi, hivyo iwapo hayatahifadhiwa yatapoteza uzalishaji wa samaki baharini.

Alisema matumbawe kwa sasa ni mazima kwa zaidi ya asilimia 80, hivyo kupitia mradi huo wanachukua jitihada mbalimbali ya kuyawekea udhibiti wa matumizi ya nyavu haramu ili yaweze kukua vizuri.

# Makamu wa Rais asimulia elimu ilivyokuwa kabla, baada mapinduzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, amesema kabla ya kutokea kwa Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1964, Zanzibar haikuwa na vyuo vikuu.

Amesema pia fursa za elimu zilitolewa kwa misingi ya ubaguzi na kuwanufaisha watoto wa wakoloni waliokuwa na uwezo wa kuwalipia ada.

Aliyasema hayo jana wakati wa ufunguzi wa maonesho ya tano ya Wiki ya Elimu ya Juu Zanzibar yaliyofanyika katika viwanja vya Maisara Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema waafrika wengi walikosa fursa ya kupata elimu kutokana na misingi ya ubaguzi pamoja na kushindwa kulipia gharama kubwa za elimu zilizokuwa zimewekwa na serikali ya kikoloni.

Hemed alisema baada ya mapinduzi hayo yalitoa fursa kubwa kwa wananchi kupata elimu bila ya malipo, ambapo azma hiyo iliyoasisiwa na Hayati Rais Abeid Amani Karume, iliendelezwa na awamu zote za uongozi kwa kuboresha miundombinu ya elimu na kukuza fursa ya upatikanaji wa elimu ngazi ya maandalizi hadi elimu ya juu.

Alisema takwimu zinaonesha kuwa hadi kufikia mwaka huu shule za sekondari zimeongezeka na kufikia 318 zikiwa na wanafunzi 110,045, ikilinganishwa na shule tano za sekondari zilizokwepo kabla ya mapinduzi zilizokuwa na wanafunzi 1,038.

Aidha, alisema hatua ya uboreshaji wa miundombinu ya elimu imetoa mafanikio makubwa ikiwemo kuongezeka kwa ufaulu kwa wanafunzi wa kidato cha nne kutoka asilimia 72.2 mwaka 202 hadi kufikia asilimia 90.9 mwaka 2023.

Alisema pia ufaulu wa kidato cha sita umeimarika kutoka asilimia 99.3 kwa mwaka 2023 hadi kufikia asilimia 99.5 kwa mwaka huu.

"Kwa upande wa fursa za elimu ya juu ambazo zilianza baada ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1964 zikiongezeka kutokana na serikali kutoa mikopo kwa wanafunzi sambamba na kuongezeka kwa vyuo vya kati, vyuo vikuu na matawi ya vyuo vikuu Zanzibar" alisema.

Alisema serikali imeongeza bajeti ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kutoka Sh. bilioni 26.95 kwa mwaka wa fedha 2023/2024 hadi kufikia Sh. bilioni 30.5 kwa mwaka fedha 2024/2025 ambazo zitawanufaisha wanafunzi 7,367, kati yao wanafunzi 4,297 wanaendelea na masomo na wanafunzi wapya 3,070 wakiwemo 1,000 kwa mara ya kwanza watafaidika na mikopo hiyo kwa ngazi ya stashahada.

Hata hivyo, aliwataka wanafunzi wanaoendelea na masomo ya elimu ya juu kuitumia vizuri fursa waliyonayo kwa kujiendeleza kielimu na kuepuka kutumika kwa misingi yoyote ambayo itapelekea kuvuruga umoja na amani ya nchi.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohamed Mussa alisema serikali inafanya kazi nzuri katika kuimarisha miundombinu ya elimu inayopelekea kuongezeka kwa kiwango cha ufaulu jambo ambalo linaendelea kuiletea heshima.

Alisema ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha sita unaongezeka mwaka hadi mwaka na kufikia asilimia 99.5 kwa mwaka 2024, ambapo zaidi ya wanafunzi 3,387 wamepata ufaulu wa daraja la kwanza hadi la tatu na wote wanatarajiwa kujiunga na vyuo vikuu ndani na nje ya nchi.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya ufunguzi wa maonesho hayo, Mkurugenzi wa shahada za awali wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Dk. Victor George alisema maonesho hayo yatawasaidia katika kufanya udahili wa vyuo na kupata taaluma juu ya kupata mikopo ya elimu juu iatakayowawezesha kusoma.

Alisema tayari chuo hicho kimefungua udahili na kwa mwaka huu wanatarajia kudahili wanafunzi zaidi ya 16,000 katika programu mbalimbali, hivyo aliwataka wanafunzi kufika katika maonesho hayo ili kufanya udahili wa elimu ya juu.

Naibu Katibu Mkuu Utawala kutoka Wizara ya Elimu, Khalid Massoud, alisema lengo kuu la maonesho hayo ni kuimarisha ushirikiano baina ya taasisi za elimu, vyuo na benki ili kuhakikisha sekta ya elimu nchini inaendelea kuimarika na kiwango cha ufaulu kinazidi kuongezeka siku hadi siku.




Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla (kushoto) akizungumza na viongozi, wa Taasisi mbalimbali za Elimu ya Juu, wanafunzi na wananchi wakati wa ufunguzi wa maonyesho ya tano ya Wiki ya Elimu ya Juu, katika viwanja vya Maisara, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Nembo maonyesho Nanenane yazinduliwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, imezindua nembo maalumu ya maonesho itakayotumika katika maonesho ya Siku ya Wakulina Duniani (Nanenane) na Siku ya Chakula Duniani.

Akizindua nembo hiyo katika viwanja vya maonesho ya kilimo Dole Kizimbani visiwani hapa, Waziri wa wizara hiyo, Shamata Shaame Khamis, alisema kuwa hatua hiyo imelenga kuongeza utoaji wa elimu kuhusu kilimo miongoni mwa jamii.

Alisema hatua hiyo itaongeza kasi katika utekelezaji wa mkakati wa mageuzi ya kilimo unaolenga kuwapatia wakulima huduma bora kama njia itakayochochea ongezeko la uzalishaji.

Alisema kuwa katika maonesho yanayofanyika Zanzibar, wakulima na wadau wa kilimo kwa kushirikiana na wataalamu wa wizara hiyo hupata fursa ya kujifunza na kubadilishana uzoefu unaostawisha sekta hiyo.

Akizungumzia shughuli na huduma zilizotolewa na wizara hiyo katika kustawisha mazao ya chakula na biashara, Shamata alieleza kuwa wizara hiyo imeendelea kutoa huduma za ugani na miche ya mazao mbalimbali yakiwemo ya biashara kwa lengo la kuongeza tija na kuondoa changamoto zinazowakabili wakulima.

Akizungumzia uzalishaji na ugawaji wa miche ya mikarafuu na nazi, alisema kwa mwaka 2023 wizara hiyo iliwapatia wakulima miche 131,000 ya karafuu kati ya miche 400,000 iliyotarajiwa kutolewa.

Kuhusu minazi, Shamata alisema kuwa idara ya kilimo ilifanikiwa kuzalisha na kutoa miche 50,000 kati ya miche 300,000 iliyolenga kuitoa na kuwaomba wakulima kuitunza miche hiyo ili lengo la kutolewa kwake lifikiwe.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA CHETI



**JOSHUA WILLSON GWAMBIYE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1571-0072** kilicholewa na **BUSEKO HILL SEKONDARI** Mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KAS/RB/280/20218**

## KUPOTEA KWA CHETI



**KULWA JULIUS MAGEMBE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S5113-0030** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ST.FRANCIS OF ASSISI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2021. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/SHI/SHI/4118/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOSEPHU ERNESTO KIBIKI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE **USAJILI T525 AJR** ILIYOPOTEA KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/10547/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**RAMADHANI HAMISI KAMBI** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye majina **WU ZHOU INVESTMENT COMPANY LIMITED** namba za usajili **MC214DEM** aina ya **HAOJUE.** Chassis No. **LC6PCJBJ9M0090929,** Engine No. **152FMIAA3R005027.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/30205/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**BAHATI KALIMA NGHWAYA** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI AINA YA KING LION 150 YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 302 DGX** YENYE CHASSIS NAMBA **LZLM15P906NHB47964.** NAOMBA YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI AU APIGE SIMU NAMBA **0786399730.** POLISI TAARIFA: **PHQ/GEI/GEI/820/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SALIM JUMA SHUMBU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 292 DZN – TOYOTA RAUM.** Chassis namba **NCZ200108551.** Engine namba **INZ0408551.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/133056/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**EUNICE AARON MADALLEH,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji yenye namba za usajili **MC 566 BRY** Chassis no **MD6M14PKXH4B62702,** Engine No OK4AH4583151. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/15545/2024.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...29/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: ADAM MRISHO MWINYIMVUA Wa MOROGORO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA NAIMA ADAM MRISHO**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 25 Mwezi 7 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

***Zingatia;***
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 18 mwezi 7 mwaka 2024

Futa isiyo...
Imetolewa leo tarehe 18 Mwezi 7 Mwaka 2024
HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO BOMA MOROGORO
HAKIMU


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.


Kwa

## Rais mpya Iran atuma ujumbe ulimwenguni

**Na Kulwa Mzee**

RAIS mpya wa Iran, Masoud Pezeshkian ametoa ujumbe kwa ulimwengu kwamba utawala wake utaongozwa na dhamira ya kuhifadhi heshima ya Kitaifa ya nchi hiyo na hadhi ya kimataifa katika hali zote.

Hayo aliyabainisha jana kwenye taarifa yake kupitia Kituo cha Utamaduni cha Jamhuri ya Kiislamu Iran kilichopo Dar es Salaam.

"Nataka kusisitiza kuwa utawala wangu utaongozwa na dhamira ya kuhifadhi heshima ya kitaifa ya Iran na hadhi ya kimataifa katika hali zote.

"Sera ya kigeni ya Iran inatokana na kanuni za heshima, hekima, busara na uundaji na utekelezaji wa sera hii ya serikali ni jukumu la rais na serikali. Ninalenga kutumia mamlaka yote yaliyotolewa kwa ofisi yangu kufuatilia lengo hili kuu,"alisema katika taarifa yake.

Aidha, alisema kwa kuzingatia hayo utawala wake utafuata sera ya kuendeshwa na fursa kwa kuunda usawa katika mahusiano na nchi zote, kwa kuzingatia maslahi yao ya kitaifa, maendeleo ya kiuchumi na mahitaji ya amani na usalama wa kikanda na kimataifa.

"Tutakaribisha juhudi za dhati za kupunguza mvutano na tutalipa imani njema kwa imani njema, chini ya utawala wangu, tutaimarisha mahusiano na majirani zetu.

"Tutashabikia kuanzishwa kwa "eneo lenye nguvu" badala ya moja ambapo nchi moja inatafuta kuhodhi na kutawala zingine, naamini kwa dhati kuwa mataifa jirani na yenye undugu hayapaswi kupoteza rasilimali zao muhimu katika mashindano yanayovunja nguvu, mbio za silaha au kuzuia bila sababu ya kila mmoja.

"Tutalenga kuunda mazingira ambapo rasilimali zetu zinaweza kuelekezwa katika maendeleo na maendeleo ya eneo kwa faida ya wote.

"Tunatarajia kushirikiana na Uturuki, Saudi Arabia, Oman, Iraq, Bahrain, Qatar, Kuwait, Umoja wa Falme za Kiarabu, na mashirika ya kikanda ili kuimarisha uhusiano wetu wa kiuchumi, kukuza biashara, kukuza uwekezaji wa pamoja, kukabiliana na changamoto za kawaida, na kusonga kuelekea kuanzisha mfumo wa kikanda wa mazungumzo, kujenga uaminifu na maendeleo,"alisema.

Mnamo Mei 19, 2024, kifo cha ghafla cha Rais Ebrahim Rais katika ajali mbaya ya helikopta kilisababisha uchaguzi wa mapema nchini Iran, kuashiria wakati muhimu katika historia ya taifa hilo.

# Joe Biden ajitenga, akutwa na Uviko-19

**WASHINTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Joe Biden, amekuwa kwenye karantini baada ya kuambukizwa Uviko -19.

Kwa taarifa ya Ikulu ya White House iliyotolewa jana ilisema kiongozi huyo ameanza kupata dalili za ugonjwa huo, lakini sio za kuhatarisha afya yake.

Mkuu wa vyombo vya habari, Karine Jean-Pierre, alisema Rais Biden, alipewa chanjo ya ugonjwa huo pamoja na ile ya nyongeza.

Alisema kuwa Biden (81) alifanyiwa uchunguzi mara mbili na kukutwa na virusi hivyo.

Kiongozi huyo wa taifa lenye nguvu duniani alionekana kwa mara ya mwisho Jumatano akiwatembelea wafuasi wa chama chake huko Las Vegas na kuzungumza katika hafla iliyokuwa imeandaliwa.

Lakini alifuta hotuba ya kampeni baadaye usiku wake.

Kugundulikana na ugonjwa huo, kunakwenda sambamba na shinikizo la kujiondoa kwenye kinyang'anyiro cha kugombea urais kwa sababu ya umri wake.

Jean-Pierre alisema rais huyo alipanga kujitenga nyumbani kwake huko Delaware huku akitekeleza majukumu yake yote kikamilifu.

Daktari wa rais, Kevin O'Connor, alisema Biden alikuwa na dalili za matatizo ya kupumua, ikiwa ni pamoja na mafua na kikohozi na alipewa dozi yake ya kwanza ya Paxlovid.

Alisema, alijisikia vizuri wakati wa hafla yake ya kwanza ya siku hiyo, lakini baadaye alipatikana na maambukizi.

Hata hivyo, Rais Biden baadaye alitumia mtandao wa X ambao zamani ulijulikana kama Twitter kumshukuru kila mtu kwa kumtakia mema na alisema atahakikisha kazi inafanyika kwa watu wa Marekani.

Vyombo vya habari vya Marekani viliripoti kwamba kiongozi wa walio wengi katika Seneti, Chuck Schumer na kiongozi wa Bunge, Hakeem Jefferies, walikutana na Biden kwa faragha na nyakati tofauti wakimsihi kujiondoa kutokana na wasiwasi wa wanachama wengi wa Democratic kuwa nafasi yake ya ugombea inaweza kuathiri ushindi.

Wakati huo huo, sakata la jaribio la mauaji ya mgombea wa Republican, Donald Trump, limechukua sura mpya baada ya ripoti kubaini kuwa mtu aliyehusika na tukio hilo alijulikana mapema baada ya kutiliwa shaka.

Ilisema idara ya Usalama na Huduma Maalum ilimfuatilia saa moja kabla ya kumfyatulia risasi Trump, lakini akapotea kwenye umati wa watu.

Maofisa wa usalama pamoja na Huduma Maalum ya Usalama walitoa taarifa hiyo kwa Bunge na Seneti kuhusu kile kilichotokea wakati wa shambulizi hilo lililotokea kwenye mkutano mjini Pennsylvania.

Seneta wa Wyoming, John Barrasso, alisema Huduma Maalum ya Usalama iliwaambia kwamba walimwona mshambuliaji saa moja kabla ya shambulio hilo, lakini akawapotea machoni.

"Alitambuliwa kama anayetiliwa mashaka kwa sababu alikuwa na chombo cha kukadiria umbali kwa matumizi na kamera au bunduki na mkoba mgongoni.

"Kwa hiyo, unaweza kutafakari, kwa muda wa saa nzima, usimpoteze mtu huyo machoni." Alihoji.

**BBC**



Baadhi ya polisi wa kikosi cha kwanza kutoka Kenya baada ya kutua uwanja wa ndege wa Toussaint Louverture nchini Haiti hivi karibuni. **PICHA: AP.**

# Polisi yapiga marufuku maandamano Kenya

**NAIROBI,** Kenya

JESHI la polisi nchini Kenya limepiga marufuku maandamano kufanyika katikati ya jiji la Nairobi hadi itakapotangazwa tena.

Taarifa iliyotolewa na jeshi hilo, ilisema limechukua hatua hiyo baada ya kubaini makundi ya wahalifu yamejiingiza kwenye maandamano hayo

Kauli ya polisi ya kuyapiga marufuku maandamano hayo imetolewa baada ya wiki kadhaa za maandamano ya kuipinga serikali.

Mkuu wa Jeshi la Polisi, Kanja Kiricho, katika taarifa yake iliyotolewa juzi ilieleza kuwa lilipata taarifa za kuaminika za kiitelijensia kuwa, makundi ya kihalifu yanapanga kuyatumia maandamano yanayoendelea kufanya mashambulizi yakiwa ni pamoja na uporaji.

Aliongeza kuwa maandamano hayo pia yamepigwa marufuku katika maeneo yanayozunguka eneo la biashara jijini Nairobi ili kuhakikisha usalama wa umma.

Awali, wanaharakati walitoa wito kwa watu kukusanyika Alhamisi katika viwanja vya Uhuru wakati polisi wakitanda katikati mwa Nairobi.

Wanaharakati hao walisema kuwa wanamtaka Rais William Ruto, kuachia ngazi.

Pia, alitoa wito wa kutaka mageuzi ili kushughulikia ubadhirifu, na utawala mbovu.

Watu wasiopungua 50 wameuwawa tangu yalipoanza maandamano yanayoongozwa na vijana mwezi mmoja uliopita.

Maandamano hayo yalianza kwa kwa kupinga muswada tata wa fedha uliotoa mapendekezo ya kuongeza ushuru lakini yaliendelea licha ya Rais William Ruto, kuuondoa mswada wa fedha wa 2024 na kulivunja baraza la mawaziri.

Maandamano hayo yaliyoratibiwa kwa njia ya mtandao bila ya uungwaji mkono kutoka kwa wanasiasa wa vyama vya upinzani, yametengeneza mgogoro mkubwa katika miaka miwili ya uongozi wa Ruto.

Wiki iliyopita, Rais William Ruto, aliahidi kuunda serikali ya kitaifa lakini muungano wa vyama vya upinzani ulikataa wazo hilo na badala yake unataka utawala unaofuata katiba.

Ofisi yake, ilipanga kufanya mazungumzo na sekta mbalimbali wiki hii ili kuyashughulikia manung'uniko ya waandamanaji lakini hadi kufikia jana, hakukuwa na dalili ya kuanza kwa majadiliano hayo.

Katika hatua nyingine, mamlaka ya mawasiliano ya Kenya imevitahadharisha vyombo vya habari dhidi ya kuchochea vurugu katika matangazo yao yanayohusu maandamano.

Mamlaka hiyo kupitia Mkuu wake, David Mugonyi, ilisema kufanya hivyo kunaweza kusababisha machafuko ndani ya taifa hilo.

**DW**

# PAMBA YASAJILI 18 WAPYA, YAJICHIMBIA KAMBINI MORO

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Pamba FC, imesajili jumla ya wachezaji 18 wapya ambao itawatumia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano mengine msimu ujao.

Meneja wa timu hiyo, Ezekiel Ntibikeha, amesema jana kuwa, pamoja na kusajili idadi hiyo ya wachezaji, lakini bado hawajamaliza kwani kuna wachezaji wengine ambao watawasili kambini siku chache zijazo.

Pamba, ambayo imepanda daraja na msimu ujao itacheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza baada ya miaka 23, imepiga kambi Morogoro kwa ajili maandalizi ya mwanzo wa msimu mpya.

“Tumekubaliana wote kuwa kambi ifanyike hapa Morogoro, tumefika hapa makocha pamoja na wachezaji wapya, tuna wachezaji wote wa zamani ambao tulihitaji kuwabakisha, lakini tuna asilimia 90 ya wachezaji wapya tuliowasajili, bado hatujamaliza, vyumba vingine vitaingia karibuni,“ alisema meneja huyo.

Wachezaji waliosajiliwa na kutambulishwa ni, Kelvin Nyanguge kutoka kikosi cha vijana cha Prisons, Ally Ramadhani na Samson Madeleka kutoka Mashujaa FC, Paulin Kisindi, akisajiliwa kutokea Coastal Union, golikipa Ally Kamtewe (KenGold), Kenneth Kunambi akitokea Singida Black Stars, na Mukenya Ally.

Wengine ni Yunus Lema kutoka Future Stars Academy, Costantine Almisu na Saleh Masoud kutoka Zanzibar, Erick Okutu na Benny Nakibinde wote kutoka Tabora United, golikipa, Yona Amos (Prisons), ambaye pia alikuwa anatakiwa na Yanga kabla ya kumsajili Khomeiny Aboubakar.

Wachezaji wengine ni Ibrahim Abdallah Abrahman kutoka Prisons, Justin Omar Bilal na Frank Ng'amba.

## SAFARINI...



Wachezaji wa Yanga, Khalid Aucho (kushoto) na Kennedy Musonda wakipozi katika picha wakati wa safari yao kuelekea Afrika Kusini jana kwa mwaliko wa mechi za kirafiki. **PICHA: YANGA**

## Wanawake 400 kupewa bima tamasha la mwanamke afya 2024

**Na Romana Mallya**

WANAWAKE 400 wa Tanzania Bara na Visiwani, watapatiwa bima ya afya bure kupitia Tamasha la Mwanamke Afya Run Run 2024, imeelezwa.

Msimamizi wa tamasha hilo, Boniface Tamba, jana alisema litafanyika siku ya nane nane katika viwanja vya Posta, Dar es Salaam.

Alisema awamu ya kwanza ya tamasha hilo walitoa bima za afya 250 na sasa wameziongeza hadi kufikia 400.

“,Mwanamke afya run sport and sports bonanza', mwaka huu itatoa kadi za afya 350 Tanzania Bara na 50 Visiwani Zanzibar,” alisema.

Tamba alisema siku hiyo kutakuwa na michezo mbalimbali ikiwamo mbio za kilometa tofauti, michezo ya jadi ambayo ni rede, karata, kufukuza kuku, kukimbia na limao kwa kijiko na kutatolewa zawadi kwa washindi ambazo zitatangazwa hapo baadaye.

Mkurugenzi wa Mwanamke Afya Athletics, Asmin Kihemba, ambaye ni mwanzilishi wa mwanamke afya, alisema mgeni rasmi anatarajiwa kuwa ni Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) na Mjumbe wa Halmashauri Kuu CCM Taifa, Mary Chatanda.

Alisema pamoja na mambo mengine, kutakuwa na upimaji wa afya na kutoa kadi hizo za afya kwa wanawake wenye kipato cha chini.

Mratibu wa tamasha hilo, Pamela Mwakasagule, alisema hakutakuwa na kiiingilio na kuomba wanawake na wanaume kushiriki kwa wingi.

# Straika Simba SC atua Mashujaa FC

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA kile kinachoonyesha haitaki kufanya makosa msimu ujao wa Ligi Kuu, Klabu ya Mashujaa, imeendelea kujiimarisha siku hadi siku kwa kufanya usajili, safari hii ikimtwaa straika wa zamani wa Simba, Mohamed Mussa.

Kocha Msaidizi wa klabu hiyo, Hussein Bunu, juzi alimesema wanaendelea kufanya usajili makini kwa ajili ya kukiimarisha kikosi ili kiwe cha kutisha msimu ujao.

“Tumeendelea kuboresha kikosi chetu, tunaamini kwa sasa tutakuwa na kikosi bora sana, kitakachoshindana kama si kuwania ubingwa basi hata tumalize ndani ya nne bora,“ alisema straika huyo wa zamani wa JKT Ruvu.



Straika huyo kinda, amemaliza mkataba wake na Simba, ambayo ilimsajili Januari, kipindi cha dirisha dogo kwenye Ligi Kuu msimu wa 2022/23, akitokea klabu ya Malindi ya Zanzibar.

Hata hivyo, alikuwa na changamoto ya kupata namba kwenye kikosi cha kwanza na hadi anamaliza mkataba wake alikuwa amefunga bao moja tu.

“Ni straika mzuri na kijana, hivyo atatusaidia sana, ataungana na mastraika tuliowasajili sasa kama Ismail Mgunda na wale wa zamani kuunda kikosi imara,“ alisema.

Mussa anakuwa mchezaji wa saba kati ya wachezaji wapya waliosajiliwa, ambapo mbali na yeye na Mgunda, wengine ni Mathew Michael, Carlos Protas, Robert Mathias Makidala , Yusuph Dunia na Ally Nassor ‚Ufudu'.

Hata hivyo, Mashujaa imeondokewa na baadhi ya wachezaji wa kutegemewa walioisaidia timu hiyo kubaki Ligi Kuu mwishoni mwa msimu uliopita ambao ni Reliants Lusajo, anayetajwa kujiunga na Dodoma Jiji, Adam Adam, aliyetambulishwa rasmi na Azam FC, pamoja na Omari Omari, ambaye kwa sasa yupo Ismailia nchini Misri akiwa na kikosi cha Simba.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MORATA KUTUA MILAN
KLABU ya Atletico Madrid inatarajiwa kuipa AC Milan idhini ya kumsajili Alvaro Morata mwenye umri wa miaka 31, wiki ijayo baada ya kukamilisha majukumu yake ya Kimataifa na Hispania kwenye Euro 2024. (***Calciomercato***)

### GATTI AITAKA JUVE
EVERTON, West Ham na Newcastle United, zinatazamiwa kumkosa Federico Gatti mwenye umri wa miaka 26, huku mlinzi huyo wa Italia akiwa tayari kuweka hatima yake kwa Juventus. (***Tuttosport***)

### WILLIAMS AWAHIWA BARCA
BARCELONA wamewasilisha pendekezo lao kwa winga wa Athletic Bilbao, Nico Williams mwenye umri wa miaka 22, katika juhudi ya kuafikiana na Mhispania huyo kabla ya klabu yoyote ya Ligi Kuu England kufanya hivyo. (***Fabrizio Romano***)

### WAN-BISSAKA NA WEST HAM
KLABU ya West Ham imepiga hatua katika mazungumzo ya kumsajili Aaron Wan-Bissaka mwenye umri wa miaka 26, kutoka Manchester United. (***Teamtalk***)

### EDERSON OFA NENE
KLABU ya Manchester City imepokea dau la pauni milioni 25 kutoka kwa Saudi Pro League kwa ajili ya mlinda mlango wa Brazil, Ederson, 30. (***HITC***)

### LINDELOF SASA SOKONI
MANCHESTER United wanataka kumuuza mlinzi wa Sweden, Victor Lindelof mwenye umri wa miaka 29, msimu huu wa majira ya joto na pia watasikiliza ofa kwa ajili ya kiungo wa kati wa Denmark, Christian Eriksen, 32. (***Manchester Evening News***)

### CHELSEA, BAYERN VITANI
CHELSEA ipo tayari kumenyana na Tottenham Hotspur, Bayern Munich na Paris St-Germain kumnunua kiungo wa kati wa Rennes, Mfaransa Desire Doue, 19. (***L'Equipe***)


### TONEY AWANIWA UNITED
KLABU ya Manchester United inavutiwa na mshambuliaji wa Brentford na England mwenye umri wa miaka 28, Ivan Toney, ambaye yuko tayari kuhamia Old Trafford. (***Christian Falk via Mail***)

### VARANE HUYOOO COMO
KLABU ya Como ya Italia iko tayari kumsajili mlinzi wa Ufaransa, Raphael Varane mwenye umri wa miaka 31, kama mchezaji huru baada ya kuondoka kwake Manchester United msimu huu. (***Fabrizio Romano***)

### WEST HAM KWA BERGWIJN
KLABU ya West Ham imeonesha nia ya kutaka kumnunua winga wa Uholanzi, Steven Bergwijn mwenye umri wa miaka 26, lakini Marseille na Klabu za Saudi Arabia pia zinatumaini kumnasa kutoka Ajax. (***De Telegraaf***)

### HODGE KUNG'OLEWA WOLVES
KLABU ya Huddersfield Town iko kwenye mazungumzo ya kumsajili kiungo wa Wolves, Joe Hodge mwenye umri wa miaka 21, baada ya mchezaji huyo wa Kimataifa wa Jamhuri ya Ireland ya chini ya miaka 21, kuchezea Queens Park Rangers kwa mkopo msimu uliopita. (***Football Insider***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MBAPPE: SIHOFII KUCHEZA NA VINICIUS JR REAL MADRID

**MADRID,** Hispania

MCHEZAJI aliyesajiliwa na Real Madrid katika majira haya ya joto, Kylian Mbappe, amesisitiza kwamba hatakuwa na tatizo kucheza na mshambuliaji wa kikosi hicho ambaye amemkuta, Vinicius Jr.

**Nahodha huyo wa Ufaransa, amesema haitokuwa changamoto kucheza na Vinicius Jr katika timu moja kwa kuwa wachezaji wazuri huwa na tabia ya kucheza pamoja.**

●●● Ni mchezaji mzuri na nina furaha kucheza naye, wachezaji wazuri wameumbwa kucheza pamoja...

Mbappe amesema: „Vinicius ni mchezaji mzuri na nina furaha sana kucheza naye. Pia, Rodrygo na kila mtu. Wachezaji wazuri wameumbwa kucheza pamoja," alisema Mbappe.

"Sitakuwa na tatizo kucheza na Vinicius. Alikuwa na misimu bora kabisa pamoja na msimu ulioisha.

„Kwangu inanibidi nibadilike na kucheza pamoja na Vinicius na Rodrygo ili tusaidiane kuleta ushindi kwa timu yetu."

## HABARI MICHEZO

# YAMAL KUIKOSA ZIARA YA MAREKANI




**BARCELONA,** Hispania

LAMINE Yamal anakaribia kukosa ziara ya Barcelona ya kujiandaa na msimu mpya nchini Marekani baada ya kuisaidia Hispania kutwaa ubingwa wa Euro.

Yamal mwenye umri wa miaka 17, alitoa asisti ya bao la kwanza kwenye fainali wakati Hispania ilipoilaza England mabao 2-1 mjini Berlin na alitajwa kuwa Mchezaji Bora Chipukizi wa Mashindano hayo nchini Ujerumani.

Fowadi huyo, ambaye alicheza mechi yake ya kwanza akiwa na umri wa miaka 15, sasa ana haki ya kupata mapumziko ya siku 21, kwa makubaliano yaliyoratibiwa na Chama cha Wanasoka wa kulipwa wa Hispania (AFE]) na mechi ya kwanza ya Barca nchini Marekani itakuwa dhidi ya Manchester City Julai 30 mjini Orlando.

Timu hiyo ya Katalunya itacheza na Real Madrid Agosti 3, huko New Jersey kabla ya kumaliza ziara yao kwa kucheza na AC Milan Agosti 6, mwaka huu, huko Baltimore.

Yamal ametuzwa kwa uchezaji wake mzuri tangu alipojiimarisha Barca na jezi namba 19 iliyokuwa ikivaliwa na Lionel Messi kati ya mwaka 2005 na 2008.

Alicheza msimu uliopita akiwa na usajili wa timu za vijana, lakini alicheza mechi 50 kwenye kikosi cha kwanza.

Yamal alicheza na jezi namba 27 mwaka jana alipokuwa akisajiliwa na timu ya vijana ya Barcelona, lakini wachezaji wote wa kikosi cha kwanza kwenye LaLiga wanatakiwa kuvaa namba zisizozidi 25.

Ushiriki wa Yamal kwenye Euro 2024, ambapo alifunga bao moja na kusaidia mengine manne, ulikamilika Jumapili iliyopita huku Hispania ikinyanyua kombe hilo kwa mara ya nne.

Kisha akarejea Madrid pamoja na wachezaji wenzake wa kimataifa siku ya Jumatatu kukutana na Mfalme wa Hispania, Waziri Mkuu wa nchi hiyo na kuendeleza sherehe pamoja na mashabiki.

Jumanne, alikuwa amerejea Barcelona, ambako alitimiza ahadi mbalimbali za kibiashara, ikiwa ni pamoja na ziara ya kazi ya uundaji upya iliyokuwa ikifanyika Spotify Camp Nou pamoja na kocha mpya, Hansi Flick na wachezaji wenzake Pedri na Gavi.

## Thiago arejea rasmi Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona imethibitisha kwamba Thiago Alcantara atajiunga kwa muda na klabu hiyo katika benchi la ufundi.

Mchezaji huyo wa zamani wa Barcelona, ataungana na Hansi Flick, kocha ambaye aliwahi kumfundisha akiwa Bayern Munich.


Thiago atahudumu katika klabu hiyo kwa muda mfupi hususan katika maandalizi ya msimu mpya.

Kiungo huyo wa zamani wa Liverpool atasafiri pamoja na kikosi cha ‚Blaugrana' hadi nchini Marekani ambapo Barcelona itacheza michezo ya kirafiki na Manchester City, Real Madrid na Ac Milan.

Thiago mwenye umri wa miaka 33, aliichezea Barcelona zaidi ya michezo 100 baada ya kuhitimu katika shule ya La Masia, kisha akatimkia Bayern Munich ambako alicheza kwa mafanikio makubwa, baada ya hapo alikwenda kumalizia maisha yake England katika Klabu ya Liverpool.




# United yakaribia kumnasa Yoro



**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inakaribia kushinda ushindani kutoka kwa Real Madrid kwa kumsajilia Leny Yoro kwa pauni milioni 51 baada ya beki huyo wa Lille kupata kibali cha kusafiri kwenda Old Trafford kwa uchunguzi wa kimatibabu, vyanzo vimeiambia ESPN.

United, ambao walikamilisha usajili wa pauni milioni 35.8 wa fowadi wa Uholanzi, Joshua Zirkzee, kutoka Bologna mapema wiki hii, wamesonga mbele ya Madrid katika mbio za kuipata saini ya Yoro, vyanzo viliiambia ESPN.

Yoro mwenye umri wa miaka 18, hapo awali alipendelea kuhamia Madrid na alikuwa akipinga uhamisho wa kwenda United, lakini klabu hiyo ya England sasa imepata mafanikio katika mazungumzo na Lille na mchezaji huyo.

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba Yoro aliiambia Madrid kuhusu nia yake ya kusaini United Jumanne usiku baada ya klabu hiyo ya Hispania kushindwa kuchukua hatua ya kumsajili.

Madrid, kama ESPN imeripoti, wamekuwa wakiwasiliana mara kwa mara na Yoro kwa miezi, lakini hawakuwahi kutoa ofa thabiti ya kumsajili. Klabu hiyo ilikuwa na Yoro kama moja ya malengo yao ya kipaumbele ili kuimarisha safu ya ulinzi baada ya kuondoka kwa Nacho, lakini vyanzo vimesisitiza kila mara kwa ESPN kwamba hawataingia kwenye vita vya ofa kwa huduma yake.

Kwa hakika, Madrid walikuwa na matumaini kwa sababu nia ya Yoro ilikuwa ni kujiunga na Madrid, lakini klabu haikuwa tayari kufikia bei iliyotolewa na United kwa mchezaji ambaye angepatikana bure ndani ya miezi 12 tu.

Lille, ambao walimaliza katika nafasi ya nne kwenye Ligue 1 msimu uliopita na kujihakikishia nafasi ya kufuzu kwa raundi ya tatu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya 2024-25, wamekubali ombi la United na Yoro sasa anasafiri kwenda Manchester kujadili masuala binafsi na kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu.

HABARI MICHEZO

## Lawi huyooo Ubelgiji...

INATOKA UK. 24

kezo haraka, nina maana wanafundishika kwa urahisi, hiki pia kimenivutia sana," alisema kocha huyo.

Kuelekea msimu ujao, Simba imesajiliwa wachezaji wengi wa ndani na nje kuanzia miaka 18 hadi 25, ikiacha idadi kubwa ya wachezaji ambao umri wao umeanza kuwatupa mkono.

Wakati huo huo, kikosi hicho kitacheza mechi ya kwanza ya Ngao ya Jamii dhidi ya watani zao wa jadi, Yanga, Agosti 8, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa jana na TFF, mechi hiyo itachezwa saa 1:00 usiku, baada ya mechi ya nyingine kati ya Azam dhidi ya Coastal Union itakayopigwa siku hiyo hiyo, saa 10:00 jioni, Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar.

## Yanga yaenda Sauzi na Baleke

INATOKA UK. 24

songa mbele ili kuungana na wenzake kuingia milango ya uwanjani hapo kabla ya safari kuanza.

Alikuwa amevaa jezi ya njano, kaptura nyeusi na raba nyeupe, akionekana kutembea haraka haraka kukwepa macho ya watu pamoja na wanahabari.

Pamoja na kuwapo tetesi kwenye vyombo mbalimbali vya habari kuwa straika huyo wa zamani wa Simba, raia wa Jamhuri ya Kidemikrasi ya Congo, kuwa na mpango wa kujiunga na Yanga, huku vingine vikisema wameshamalizana, lakini hadi leo klabu hiyo haijatangaza lolote kuhusu usajili huo.

Kuonekana kuwa kwenye kundi la wachezaji walioondoka kwenda Sauzi, kunadhihirisha kuwa mchezaji huyo wakati wowote klabu hiyo itamtangaza rasmi kuwa mchezaji wao.

Straika huyo alijiunga na Simba 2023 na aliachwa 2024, akarejea klabu yake ya TP Mazembe inayommiliki, ambao nao walimtoa tena kwa mkopo katika Klabu ya Al Ittihad ya Libya.

Ofisa Habari wa Klabu ya Yanga, Ali Kamwe, amesema kikosi kimeondoka kwa mialiko miwili tofauti.

Alisema kutakuwa na michuano maalum ya Mpumalanga na ile ya Kombe la Toyota ambayo ilihabarishwa siku chache zilizopita.

"Niwaambie tu wanachama na mashabiki wa Yanga, hii siyo ‚pre season‘, sisi kambi yetu ya maandalizi itakuwa pale pale Kigamboni, lakini kilichobadilika ni kwamba wakati huu wa ‚pre seasons‘, kila nchi na klabu zinaanda mashindano maalum ya kujipima nguvu kabla ya mashindano kuanza, hivyo tumepokea ofa nyingi za klabu kutualika.

"Tumekubali mialiko miwili tu, moja ni ya timu ya TS Galaxy ya Mpumalanga ambayo inashiriki Ligi ya Afrika Kusini, pale kuna mashindano ambayo pia tumealikwa na tulishawatangazia ya Kombe la Toyota," alisema.

# BAJANA AKATAA KUBEBWA NA KANUNI, ATAKA KUPAMBANA

**Na Adam Fungamwango**

SIKU chache baada ya rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Wallace Karia, kusema hawatopunguza wachezaji 12 wa kigeni kama ambavyo ilipendekezwa na baadhi ya wadau wa soka kwenye maboresho ya kanuni ya msimu ujao, mchezaji wa Azam FC, Sospeter Bajana, amewaibukia na kuwataka wachezaji wenzake wa Kitanzania kupambania namba na si kutegemea kanuni kwani itawashushia hadhi.

Akizungumza akiwa nchini Morocco ambako kikosi cha Azam FC kimeweka kambi kwa ajili ya msimu ujao wa mashindano, Bajana alisema wachezaji wa Kitanzania kama watajitambua, wanaweza kupata namba kwenye kikosi chochote kile nchini na kuwapiku wanaotoka nje.

Alisema atafurahi kuona mchezaji wa Kitanzania anacheza kutokana na kiwango chake anachokionyesha uwanjani na kukubalika na kocha, badala ya kupangwa kwa sababu ya kubebwa na kanuni.

"Mjadala nimeusikia, mimi sidhani kama sisi wenyewe wachezaji linatusumbua sana, ni kiasi cha mchezaji mwenyewe kujitambua kujua nini anafanya uwanjani, tukiweza kupambana na kuwaweka nje wachezaji wa kigeni, itatupandisha thamani, mfano akiletwa mchezaji ambaye kiwango kiko juu na wewe inabidi upandishe kiwango chako," alisema kiungo huyo mkabaji.

Aliwaasa wachezaji wenzake kwamba kupambana kutawasaidia wao wenyewe na familia zao na si kwa ajili ya klabu pekee.

"Naawambia tu wachezaji wenzangu, akiletwa mchezaji kutoka nje ni lazima apambane kuwania nafasi kwa sababu hiyo itamsaidia yeye mwenyewe kwanza kuborosha kiwango chake ili hata klabu za nje ziweze kummezea mate.

„Ataisaidia klabu yake kupata ushindi, pia atalisaidia taifa kwani kiwango chake kitamfanya kuitwa Taifa Stars na atakuwa ni mchezaji aliyeitwa kwa ubora, si kwa sababu anapewa nafasi ya kucheza kwa kanuni," alipigilia msumari.

Naye winga wa timu hiyo raia wa Gambia, Gibril Sillah, aliwataka wachezaji wa Kitanzania kutowaogopa, kwani hata wao wanalazimika kupambana kupata namba kwa kuwa wanatoka nje ya nchi na kukuta kuna wachezaji wengi wazawa ndani ya kikosi, hivyo nao wanakuwa na hofu kama hiyo, lakini hawalalamiki zaidi ya kupambana.

"Kwangu mimi nawashauri wachezaji wa Tanzania, mfano Azam ina wachezaji 12 wa kigeni, waliobaki wote ni wazawa, sasa kama unataka kucheza basi unapaswa kufanya kazi, na hata sisi wachezaji wa kigeni tunafanya kazi sana, maana ukiona mchezaji wa Kitanzania anakuweka benchi, basi lazima uwe na tahadhari kwani unaweza kuondoka muda wowote, hivyo ni lazima upambanie nafasi yako," alisema.

MAISHA MAPYA...




Kylian Mbappe (katikati) akipozi katika picha na wazazi wake, Wilfried Mbappe na Fayza Lamari, wakati akitambulishwa juzi na klabu yake mpya, Real Madrid. Mbappe amesajiliwa na Real Madrid majira haya ya joto kwa uhamisho huru baada ya kumaliza mkataba wake na PSG. **PICHA: MTANDAO**

# Karia akunwa ushindani Dar Port Kagame Cup

**Na Shufaa Lyimo**

BARAZA la Vyama vya Michezo Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), limezipongeza timu zinazoshiriki mashindano ya Dar Port Kagame Cup kutokana na ushindani unaonyeshwa, ambapo michezo ya nusu fainali itapigwa leo kwenye Uwanja wa KMC pamoja na Azam Complex.

Mchezo wa mapema utachezwa majira ya saa 9:00 alasiri katika Uwanja wa KMC, ambao utazikutanisha APR (Rwanda) dhidi ya Al Hilal FC (Sudan), huku wa pili ukipigwa saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Azam Complex, ukizikutanisha Al Wadi FC (Sudan) dhidi ya Red Arrows ya Zambia.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, rais wa CECAFA, ambaye pia ni rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, alisema mashindano hayo yamekuwa na mvuto kutokana na upinzani uliopo na kuahidi kuyaboresha zaidi hapo mwakani.

"Mashindano haya yanazisaidia timu kufanya maandalizi kwa ajili ya kujiandaa na msimu ujao pamoja na yale ya kimataifa, ninaahidi kuyaboresha zaidi hapo mwakani," alisema Karia.

Rais huyo alisema mwaka huu wameshindwa kuziingiza timu hatua ya robo fainali na moja kwa moja kucheza nusu fainali kutokana na kuwapo kwa changamoto ya uwezeshwaji, baada ya kusimama kipindi kirefu bila kufanyika.

Wakati huo huo Afisa Mtendaji Mkuu wa CECAFA, Auka Gecheo, alisema fainali ya mashindano hayo itafanyika kwenye Uwanja wa Azam Complex Jumapili wiki hii.

"Timu zote ambazo zinashiriki mashindano haya zimeonyesha uwezo mkubwa hali iliyochangia kuwa na mvuto tunaomba mashabiki waje kwa wingi Jumapili kushuhudia fainali," alisema Gecheo.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano, Alhaji Mgoyi, aliushukuru uongozi wa CECAFA kwa juhudi iliyofanya na kufanikiwa kuyarudisha.

Michezo
Ijumaa Julai 19, 2024
Nipashe



## Yamal kuikosa ziara ya Marekani

UK. 22

SURA ZA KAZI...



Wachezaji wa Simba wakiwa mazoezini huko Ismailia, Misri, kujiandaa na msimu mpya wa 2024/25. **PICHA: SIMBA**

## Yanga yaenda Sauzi na Baleke

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha wachezaji wa Yanga kimeondoka nchini jana mchana kwenda nchini Afrika Kusini kucheza mechi kadhaa za kirafiki pamoja na michuano ya Kombe la Toyota, kikiongozana na straika wa zamani wa Simba, Jean Baleke.

Baleke alionekana jana akiwa pamoja na wachezaji wa Yanga waliokuwa wakisafiri na kikosi hicho, ingawa mwenyewe hakutaka kuonekana.

Alivaa kofia ambayo ilificha karibu asilimia 90 ya sura yake, pamoja na spika za masikioni ikionekana wazi lengo lilikuwa ni kutovutia wanahabari na watu waliofika kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Julius Nyerere, hata hivyo haikuwa kama alivyotarajia.

Badala yake alitambulika kiurahisi na kuwa ndiye kivutio pekee uwanjani hapo, akifuatwa yeye na wanahabari wakimuuliza maswali kadhaa, lakini hakujibu chochote zaidi ya ku-

INAENDELEA UK. 23

# LAWI HUYOOO UBELGIJI, FADLU AKOSHWA SIMBA

### ●●● Ataja mambo matatu utamu wa kikosi chake huku akieleza wanafundishika kirahisi na...

**Shufaa Lyimo na Adam Fungamwango**

HUKU sakata lake likiwa bado halijaamuliwa, mchezaji ambaye amezua sintofahamu kati ya Simba na Coastal Union, Lameck Lawi, muda wowote kuanzia sasa anatarajiwa kuelekea nchini Ubelgiji kwa masuala yake binafsi, imeelezwa.

Simba ilipeleka shauri lake kwa Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuhusu kuvunjiwa mkataba na Coastal Union wa kumsajili beki Lawi kungali walishafanya biashara na kukamilisha malipo, lakini wauzaji wa mchezaji huyo wakazirejesha wakidai malipo yalifanywa baada ya muda wa makubaliano kupita.

Hata hivyo, shauri hilo lilisikilizwa Jumanne wiki hii, kwa pande zote kutoa vielelezo, lakini bado halijatolewa uamuzi wa nani hasa anapaswa kummiliki mchezaji huyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Msemaji wa Coastal Union, Abbas El Sabri, alisema baada ya kurejea Tanga mchezaji huyo aliomba ruhusa ya wiki moja kwa ajili ya safari yake ya Ubelgiji.

**"Kwa sasa Lameck hayupo kambini ameomba ruhusa ya wiki moja kuelekea nchini humo, kwa mujibu wa ruhusa yake anatakiwa awapo kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii utakaochezwa Agosti 8, mwaka huu, dhidi ya Azam FC," alisema El Sabri.**

Alisema kwa sasa wanasubiri maamuzi yatolewe na Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya TFF kutokana na sakata la mchezaji wao huyo dhidi ya Simba.

Katika hatua nyingine, wakati hayo yakiendelea kikosi cha Simba chenye sura mpya ngingi kinaendelea na maandalizi ya msimu mpya mjini Ismailia, Misri na tayari Kocha Mkuu wa timu hiyo, Fadlu Davids, amekuwa na nyota wake kwa ujumla.

Fadlu amekimwagia sifa kikosi chake, akisema kinafundishika kwa urahisi, huku akifurahishwa na uwezo, kasi na nguvu kwa wachezaji wake.

Akizungumza jana akiwa jijini Ismailia, kocha huyo alisema wiki moja tu baada ya kuwapa mazoezi ameridhishwa kwa kiasi kikubwa na kikosi cha wachezaji aliowakuta, wa zamani na wapya.

Alisema kuna mambo matatu ambayo yamemfurahisha tangu atue kutoka Raja Casablanca na kukinoa kikosi cha Simba.

"Wiki moja tu baada ya kufanya mazoezi na wachezaji wangu nimeridhika kwa kiasi kikubwa na timu niliyokuwa nayo, na sababu kubwa nimewakuta wachezaji wengi wana umri sahihi wa kucheza.

"Kwanza wapo kwenye umri sahihi wa kucheza mpira, miaka kuanzia 19 hadi 25 ndiyo umri wa mchezaji kuwa kwenye kiwango cha juu sana, wachezaji wa aina hiyo ndiyo wamejaa hapa.

"Pili nimefurahishwa na kasi nguvu walizonazo wachezaji wangu, nadhani hii pia ni sababu ya umri, kwa hiyo wanaweza kucheza soka la kuvutia, lakini pia wanaweza kucheza soka la kutumia nguvu zaidi, kwa maana hiyo wanaweza kucheza katika mazingira yoyote, hivyo kunipa uwanja mpana wa jinsi ya kucheza mechi husika, au kulazimika kucheza kutokana na mpinzani anavyocheza," alisema kocha huyo.

Kingine alisema ni uwezo wao wa kupokea maelekezo haraka, ambapo inarahishia kazi kwenye kukinoa kikosi hicho.

"Tatu ni uwezo wa wachezaji kupokea maele-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >